# Nipashe

Jumamosi Machi 28, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580191

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




## Wakala wa ukatishaji tiketi afariki kwa kukanyagwa akikimbilia basi

UKURASA 3




UKURASA 13

# Corona yaponza mume na mkewe

• **Watiwa** mbaroni tuhuma kuikejeli serikali, wadaiwa kusema haina pesa kisa kufunga shule, vyuo... *Endelea ukurasa 2*



Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, SACP Lazaro Mambosasa, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akitangaza kukamatwa kwa watu wawili mme na mke, waliokuwa wakiidhihaki serikali kuhusu ugonjwa wa corona. **PICHA: JUMANNE JUMA**



### BAA LA CORONA

**WAZIRI Mkuu wa Uingereza, Borris Johnson, amekutwa na virusi vya corona baada ya kufanyiwa vipimo huku Afrika Kusini ikiripoti vifo vya watu wawili kutokana na ugonjwa huo. Chukua tahadhari!**

- **Epuka mikusanyiko ya watu**
- **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
- **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
- **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

## Lipumba ajitetea kwa hoja za CAG

UKURASA 3

## Mwalimu mstaafu alipa mil. 45/- mkopo mil. 3/-

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



**MICHEZO** **SENZO: SIMBA ITASAJILI KISASA** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Mwalimu alipa mil. 45/- kwa mkopo wa mil. 3/-

**Na Asha Shabani,** MUSOMA

MWALIMU mstaafu mkoani Mara, Theodosia Alphonce, amelipa Sh. milioni 45 katika taasisi moja ya fedha kutokana na mkopo wa Sh. Milioni tatu, imefahamika.

Kutokana na kushindwa kulipa kikamilifu mkopo huo, mwalimu huyo alinyanyg'anywa pia nyumba yake ambayo amerejeshewa pamoja na Sh. milioni 30 kutokana na juhudi za Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa mara.

Wakati mwalimu huyo akifanyiwa hivyo, Ofisa Elimu Mstaafu wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Pantaleo Rwiza, alikopa Sh. milioni 8.9 na wakati pesheni yake imetoka, wakopeshaji hao walichukua Sh. milioni 89.

Akizungumza jana baada ya kukabidhiwa nyumba yake na Sh. milioni 30, Mwalimu (mstaafu) Alphonce, alisema alikuwa amekopa Sh. milioni tatu lakini wakati wa malipo wakopeshaji hao walichukua Sh. milioni 45 pamoja na nyumba yake, tofauti na makubaliano ya awali.

Mwalimu huyo alisema kutokana na malipo hayo, alilazimika kutafuta haki yake Takukuru kwa kuwa jambo hilo lilikuwa kinyume cha makubaliano katika mkataba wa kukopa.

Kwa upande wake, Rwiza aliishukuru Takukuru kufanikisha Sh. milioni 55 ambazo alikuwa ametapeliwa na wakopeshaji hao.

**TAKUKURU YAFUNGUKA**

Kutokana na kubainika kwa dhuluma hizo, Takukuru Mkoa wa Mara, imesema imewabaini watumishi watatu wa idara ya elimu wanaoshirikiana na watumishi wa benki na taasisi za fedha kuwatapeli baadhi ya wastaafu wanaolimbikiziwa riba na wakopeshaji.

Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Mara, Alex Kuhanda, alisema wastaafu hao wamekuwa wakiumizwa na baadhi ya wakopeshaji hao kwa kukopa kiasi kidogo cha fedha na kuongeza riba mpaka asilimia 1,800 kwa mkopo.

Akizungumza na Nipashe wakati wa kukabidhi Sh. milioni 85 na nyumba moja ya wastaafu ambao walikuwa wamenyang'anywa mali zao, Kuhanda alisema kuanzia Desemba, mwaka jana hadi sasa, Sh. milioni 275 zimerejeshwa kutoka kwa watu hao aliowaita 'wakopeshaji umiza' na kukabidhiwa kwa wastaafu waliokumbwa na mkasa huo.

Kuhanda alisema wastaafu wengi mkoani hapa wamekuwa wakitapeliwa fedha au mali zao na wakopeshaji hao kwa kupewa mikopo ambayo mikataba yake imekuwa tofauti wakati wa malipo na kufanya wengi kuangukia katika madeni makubwa na kudhulumiwa.

Alisema wakopeshaji hao wamekuwa wakifanya dhuluma hiyo kwa kushirikiana na watumishi wa idara za serikali wakiwamo watatu kutoka idara ya elimu ambao wamebainika kushiriki kikamilifu.

**RC AONYA**

Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima, ameonya kuwa hawatamwonea aibu mtumishi yeyote anayejihusisha na mchezo huo huku akiwataka kufuata maadili ya kazi zao.

Sambamba na hilo, amewataka wastaafu wote waliotapeliwa na 'wakopeshaji umiza', kujitokeza na kudai haki yao huku akisema mkoa wake umejipanga mapema kukomesha vitendo hivyo vya dhuluma kwa wastaafu.



Mafundi wakiendelea na kazi ya ujenzi wa kuweka mabomba ya maji machafu katika eneo la Shule ya Sekondari Mama Salma Kikwete, eneo la Kijitonyama, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Corona yaponza mume, mke

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linawashikilia mume na mke kwa madai ya kutoa taarifa za uongo na za kejeli dhidi ya serikali kuhusu virusi vya corona wakati wakiwa kwenye daladala.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Kamanda wa Polisi wa kanda hiyo, Lazaro Mambosasa, aliwataja wawili hao kuwa ni Boniface Mwita (29) na Rosemary Mwita (41), wote wakazi wa Tabata jijini.

Kamanda Mambosasa alisema watuhumiwa hao walikamatwa Machi 20 mwaka huu saa saba mchana wakiwa kwenye daladala yenye namba za usajili T 119 DKS, wakitokea Tabata kuelekea Muhimbili.

"Wakiwa kwenye daladala hilo, watuhumiwa hao walianza kukejeli, wakitania kwa kusema kwamba serikali inapotosha wananchi kwamba kuna virusi vya ugonjwa wa corona.

"Na pia walisema serikali haina fedha kwa ajili ya kulisha wanafunzi ndiyo maana shule na vyuo vimefungwa kwa kisingizio cha uwapo wa corona na kwamba serikali inafanya hivyo kwa ajili ya kuomba msaada kutoka mataifa mbalimbali," alidai.

Kamanda Mambosasa alisema jambo hilo kulingana na hali halisi nchini, liliwakera abiria wenzao kwenye daladala na kuamuru kuwaweka chini ya ulinzi.

"Abiria hao walimwelekeza dereva wa daladala kulipeleka kituo cha polisi kwa ajili ya hatua, walipofika kituo cha polisi, walikamatwa upya na kuletwa Kituo Kikuu cha Polisi Kati ambako wanaendelea kushikiliwa," alisema.

Kamanda Mambosasa alisema upelelezi wa shauri hilo umekamilika na tayari jalada lake limeshaandaliwa na kupelekwa kwa Wakili wa Serikali kwa hatua nyingine ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani.

"Nipende kutoa rai na onyo kwa Watanzania ambao wanaleta mzaha na kejeli kwa ugonjwa huu ambao kimsingi unaangamiza watu duniani, Tanzania ikiwa ni sehemu ya dunia hii, ni lazima watu wapokee maelekezo kutoka kwa viongozi wa serikali. "Rais John Magufuli ameshaongea, waziri mwenye dhamana ameshaongea, kila mmoja kwa nafasi yake atambue siyo jambo la kuchukulia mzaha hata kidogo kwa sababu ugonjwa unaondoa makumi kwa maelfu," alionya.

# RC ataka udhibiti wa wageni kisa corona

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, amewataka wakazi wa mkoa huo kutoa taarifa za wageni wasiofahamika walikotoka pindi wanapoonekana katika maeneo yao ili kuepuka kuambukizwa virusi vya corona.

Amesema Tabora ni mkoa mkubwa na unapakana na mikoa inayopakana na nchi za jirani, hivyo kuna uwezekano wa wageni kuingia kwa kutumia njia za panya na kuhatarisha afya za wakazi wake.

Mwanri alisema hayo jana alipokuwa akifungua mkutano wa timu ya mkoa ya kudhibiti janga la corona kuingia mkoani hapa.

Aliwahimiza wananchi kuendelea kuchuka taadhari dhidi ya maambukizo ya ugonjwa huo kwa kunawa mikono mara kwa mara.

Pia aliwataka wananchi kususia maduka yote ambayo wamiliki wake watakutwa hawajaweka vitakasa mikono au ndoo kwa ajili ya wateja kunawa kabla ya kununua bidhaa. Mwanri alisema wamiliki wa aina hiyo wana nia mbaya na Watanzania na wanapingana na maagizo ya viongozi wa kitaifa na wataalamu ya kuwataka wananchi kunawa mikono kama kinga dhidi ya janga la corona.

Alivitaka vyombo vya habari hasa redio zilizoko mkoani hapa kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya kujikinga na corona ili mkoa uendelee kuwa salama.

# Wakala basi afa akikimbilia basi

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA MJINI

ATHUMANI Omari (38), mkazi wa Jiji la Mwanza na Wakala wa Basi la Kisbo, amefariki dunia kwa kukanyagwa na basi la kampuni hiyo lenye namba za usajili T 192 DBZ, kwenye Stand Kuu ya Mabasi mkoani Shinyanga.

Tukio hilo limetokea jana majira ya 2:30 asubuhi, wakati basi lilipoingia kwenye stendi hiyo likitokea jijini Mwanza kwenda Dar es Salaam likiwa na wakala huyo. Ilielezwa na mashuhuda tukio hilo kuwa basi hilo lilipofika katika stendi hiyo kupakia abiria, wakala huyo alishuka na wakati likiondoka, aliruka ili kuingia kwenye basi na kuteleza chini ya uvungu ndipo akakanyagwa na kufariki dunia papo hapo.

Akisimulia tukio hilo, mmoja wa mashuhuda hao, mfanyabiashara wa stendi, Joseph Thomas, alidai wakati basi hilo likiondoka, wakala huyo alilikimbilia na aliporuka kwenye mlango, aliteleza na kukanyagwa.

Alisema wakati basi likiondoka stendi, lilikuwa katika mwendo mkali na baada ya wakala huyo kukanyagwa, dereva wa basi aliteremka na kukimbia.

"Mimi nimeshuhudia kabisa huyu wakala wa basi akikanyangwa na basi la Kisbo, yaani alipokuwa anarukia kwenye basi, akateleza mlangoni na kuangukia kwenye uvungu wa basi, ndipo akakanywa na mataili na mwili wake kusambaratishwa," alisema.

Dereva wa magari kwenye stendi hiyo, Paschal Mboje, alitoa wito kwa askari wa Kikosi vya Usalama Barabarani kuzuia utaratibu wa mabasi kutoka kwa mwendokasi katika stendi hiyo na kuweka utaratibu wa kuyatoa kwa foleni.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Deborah Magiligimba, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo na kwamba mwili wa marehemu umehifadhiwa kwenye chumba cha maiti katika Hospitali ya Rufani mkoani humo.

Alisema dereva wa basi hilo, Jabu Dalueshi (45), mkazi wa Dar es Salaam, anashikiliwa na Jeshi la Polisi ambalo pia linalishikilia basi hilo kutokana na ajali hiyo.

Alitoa wito kwa madereva kuwa makini wanapoondoa mabasi kwenye stendi hiyo ili kuepuka kusababisha ajali zisizo za lazima.

# Mbaroni tuhuma kuvamia, kuiba kwa ofisa serikali

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, linawashikilia watu watano wanaodaiwa kumjeruhi ofisa wa serikali na kupora nyumbani kwake mali zenye thamani ya Sh. milioni 3.7.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Kamanda wa kanda hiyo, Lazaro Mambosasa, aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Juma John (27), mkazi wa Bungu A, Japhet Charles (25) na Victor William (23), wote wakazi wa Chanika.

Kamanda Mambosasa aliwataja watuhumiwa wengine kuwa ni Joseph Charles (28), mkazi wa Mbezi Juu na Anthony Christian (40), mkazi wa Temeke jijini.

Alisema watuhumiwa hao walikamatwa usiku wa Machi 22 mwaka huu maeneo ya Tegeta wakiwa na silaha za jadi ambazo ni mapanga na marungu.

"Watuhumiwa hawa walivamia nyumbani kwa Victor Nyirenda ambaye ni ofisa wa serikali na kumjeruhi kichwani kisha kupora simu mbili, kompyuta mpakato mbili aina ya HP, pochi na bahasha iliyokuwa na Sh. 500,000," alisema.

Alibainisha kuwa watuhumiwa hao waliiba vitu vyenye thamani ya Sh. milioni 3.7 na baada ya taarifa kulifikia Jeshi la Polisi, ufuatiliaji ulianza na kuwakamata wote.

Kamanda Mambosasa alisema juzi walikamata watuhumiwa wengine wanne waliopokea vitu vya wizi kutoka kwa wahalifu wanaofanya matukio ya uvunjaji. Alisema baada ya upekuzi kufanywa kwenye maduka ya watuhumiwa, walikamata kompyuta mpakato tatu, simu 10, luninga, deki na chaji za kompyuta.

Kamanda Mambosasa pia alisema jeshi hilo limekamata silaha mbili aina ya shotgun Pump Action na Maker Four.

Alisema silaha aina ya Shotgun Pump Action yenye namba za usajili 011822114, mali ya Kampuni ya Ulinzi ya OK Security, ilipotea katika mazingira ya kutatanisha.

Kamanda Mambosasa alisema katika tukio hilo, wamewakamata walinzi wawili wa kampuni hiyo ambao ni Akili Mlatoni (31), mkazi wa Mtoni Mtongani na Isack Junia (22), mkazi wa Mwananyamala Ujiji.

Alisema silaha hiyo iliibwa Machi 19 mwaka huu katika Kanisa la EAGT City Centre Mtoni Mtongani.

Alisema silaha ya pili imekutwa imetelekezwa katika ghala la Kampuni ya Enka Enterprises na kwa sasa wanaendelea kumsaka mmiliki wake.




Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akijibu tuhuma zilizotolewa katika taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2018/19, dhidi ya chama chake, kuhamisha fedha kutoka kwenye akaunti ya chama na kuwekwa kwenye akaunti ya mtu binafsi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Lipumba ajitetea hoja za CAG

**Na Elizabeth Zaya**

MWENYEKITI wa Chama cha Wananchi (CUF), Profesa Ibrahimu Lipumba, ameeleza sababu za chama chake kuhamishia kwenye akaunti ya mtu binafsi Sh. milioni 369 zilizotolewa na serikali zikiwa ruzuku kwa chama hicho.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Profesa Lipumba alidai mgogoro ndani ya chama hicho ndiyo uliosababisha wachukue uamuzi huo.

Alisema mgogoro huo ambao ulikuwa ndani ya chama kwa muda mrefu ukihusisha pia aliyekuwa Katibu Mkuu, Maalim Self Sharif Hamad, ulisababisha kuwapo na tishio la kuzuia pesa hizo kutumika.

Alidai kuwa Maalim Self ndiye alikuwa akitishia kufunga akaunti hizo zisitumike kwenye chama hicho upande wa Tanzania Bara. "Jana (juzi) CAG alisema alibaini CUF kupokea ruzuku toka serikalini Sh. milioni 369 na kuhamisha fedha hizo Sh. milioni 300 kutoka akaunti ya chama na kuzipeleka kwenye akaunti binafsi.

"Kauli hii ya CAG imeleta mtafaruku na sintofahamu kuhusu usimamizi wa fedha za CUF. Tukio hili la kuhamisha fedha kupeleka kwenye akaunti ya mtu binafsi lilitokea Januari 2017 wakati chama kikiwa katika mgogoro wa uongozi, na akaunti za chama katika benki ya NMB zilikuwa na tishio la kuzuiwa," alisema. Profesa Lipumba alisema kuwa mwaka 2016, aliiandikia barua kwa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini akiomba chama hicho kiruhusiwe kutumia fedha hizo kwa shughuli za kichama.

"Desemba 2, 2016, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ilitangaza uchaguzi mdogo wa ubunge Jimbo la Dimani, Zanzibar na chama kilisimamisha wagombea 14 kati ya kata 20 zilizokuwa zimetangazwa kurudia uchaguzi huo.

"Wakati uchaguzi huo unatangazwa, chama kilikuwa hakipewi ruzuku na Desemba 28, 2016, niliiandikia Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuiomba itupatie fedha zitokanazo na ruzuku ya kila mwezi ili tushiriki katika uchaguzi mdogo," alisema.

Profesa Lipumba alisema kuwa baada ya kuandika barua hiyo, Ofisi ya Msajili iliridhia kwamba chama hicho kipate sehemu ya ruzuku ili kishiriki katika uchaguzi huo pamoja na kutekeleza shughuli za chama.

"Ofisi ya Msajili iliweka fedha hizo katika akaunti ya chama Benki ya NMB, Tawi la Temeke, katika kipindi hicho kulikuwa na tishio la aliyekuwa Katibu Mkuu wa chama kuzuia akaunti zote za chama Tanzania Bara zisifanye kazi.

"Katika hali hiyo, Kamati ya Utendaji ya chama iliamua Sh. milioni 300 zihamishiwe kwenye akaunti ya mwanachama mwaminifu ili zisikwame benki.

"Sh. milioni 69 zilizotolewa na kuanza kugharimia shughuli za kampeni za uchaguzi zikiwamo ziara za viongozi kwenda kwenye kata zenye uchaguzi mdogo. "Fedha zote zilizowekwa kwenye akaunti ya mwanachama huyo zilitumiwa na chama katika masuala ya uchaguzi na uendeshaji wa masuala ya chama zikiwamo ruzuku za wilaya tunazozipeleka kila mwezi tukiwa na ruzuku," alisema.

Profesa Lipumba alisema kwamba hata baada ya wakaguzi kutoka katika Ofisi ya CAG walipkwenda kufanya ukaguzi kwenye chama hicho walielezwa yote hayo pamoja na kuwapatia nyaraka zote.

"Wakaguzi kutoka Ofisi ya CAG walipokuja kutukagua, walipewa maelezo haya na nyaraka za matumizi ya chama ya mwaka 2016/17 zikiwamo hizo za fedha Sh. milioni 369 zilizowekwa NMB Temeke,"alisema.

Alisema hatua ya kuweka fedha kwenye akaunti ya mwanachama huyo ilisaidia kukamilisha shughuli za chama kwa sababu baadaye NMB ilizuia kutoa fedha kwenye akaunti zote za Tanzania Bara.

"Sasa, mgogoro umemalizika na taratibu za fedha zinazingatia kanuni za fedha za chama na tunakubaliana na CAG kwamba mifumo ya udhibiti wa fedha ndani ya chama chetu inatakiwa iimarishwe kwa kufuata sheria na katiba ya chama.

"Na sasa hivi mhasibu wetu anaandaa mfumo imara wa udhibiti huo wa fedha ndani ya chama," Profesa Lipumba alisema.

## Kanisa lalalamika kupokwa eneo

**Na Ndalike Sonda,** KAHAMA

UONGOZI wa Kanisa Katoliki Jimbo la Kahama, umeilalamikia Idara ya Ardhi ya Halmashauri ya Mji wa Kahama kwa kile unachodai kumegwa kwa eneo linalomilikiwa na Wanawake Wakatoliki Tanzania (Wawata) jimboni humo kisha kuuzwa kwa mwanachi.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa jana, Mwenyekiti wa Wawata Jimbo la Kahama, Joyce Mhagama, alidai eneo hilo linalopakana na uwanja wa mpira wa Magereza, walilinunua tangu mwaka 1997 na walilitenga kwa ajili ya kuanzisha shule ya awali.

Alidai taarifa za kuuzwa kwa eneo lao walizipata kutoka kwa mwanamke ambaye ni muumini mwenzao aliyepita eneo hilo na kuona shughuli za kulisafisha zinaendelea na baada ya kufuatilia, waliambiwa na maofisa ardhi kwamba eneo liko nje ya eneo la kanisa.

Mwenyekiti wa Jimbo hilo, Edward Kinungu, alisema wanajiandaa kufuatilia ili eneo hilo lirejeshwe. Mwenyekiti wa zamani wa Wawata jimboni humo, Maria Kakunguru, alisema baada ya kulinunua eneo hilo walifuata taratibu zote za upimaji.

Dk. Seif Seif anayedaiwa kuuziwa eneo hilo na Halmashauri ya Mji wa Kahama, alisema atalizungumzia baadaye suala hilo atakapopata muda baada ya kupigiwa simu na waandishi wa habari.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, Anderson Msumba, alikiri kupokea malalamiko hayo na kuahidi kufuatilia ili kujua uhalali wa umiliki wa eneo hilo.

Alisema halmashauri imeshaelekeza upimaji wowote wa ardhi lazima uwe na kibali kutoka ofisi yake pamoja na uongozi wa kata husika.

# Wakusanya ushuru mbaroni madai rushwa ya 120,000/-

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Manyara, inawashikilia mawakala watatu wa kukusanya ushuru wa mazao katika Halmashauri za Mji na Wilaya ya Babati kwa tuhuma za rushwa.

Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Manyara, Holle Makungu, aliwataja mawakala hao kuwa ni Iddy Sulle wa kizuizi cha Sinai Halmashauri ya Mji wa Babati, Ezekia Thanahandi kizuizi cha Kampala Halmashauri ya Wilaya ya Babati na Basil Aloyce wa Sinai.

Alisema mawakala hao wamekamatwa kwa tuhuma za kuomba rushwa ya Sh. 120,000 kutoka kwa mfanyabiashara wa mazao (jina limehifadhiwa) aliyekuwa akisafirisha mchele, vitunguu na viazi mviringo kwa gari kutoka Singida kwenda Arusha, Machi 25, mwaka huu. "Awali mfanyabiashara huyo alipitia kizuizi cha Kampala kilichokuwa kimefunguliwa bila kuwapo kwa wakusanya ushuru. Hata hivyo, gari hilo lilipofika kituo cha Sinai lilizuiwa," alisema Makungu. Baada ya muda mfupi, alisema Sulle na Thanahandi kutoka kizuizi cha Kampala, walifika eneo hilo na kuchukua hati za kusafirishia mazao hayo huku wakimtaka mfanyabiashara huyo afuate nyaraka hizo katika kizuizi cha Kampala siku iliyofuata.

"Mfanyabiashara huyo alitii agizo hilo na kulipopambazuka alifuata nyaraka zake kizuizi cha Kampala, ndipo alipopewa sharti la kutafuta Sh. 120,000 ili kuwekewa saini kwenye nyaraka zake na hatimaye kuendelea na safari ya Arusha," alisema.

Mkuu huyo wa Takukuru alisema mfanyabiashara huyo hakuridhika ndipo alitoa taarifa katika taasisi hiyo na uchunguzi ukafanyika kujiridhisha kuhusu madai hayo kisha fedha za mtego zikaandaliwa ambazo ziliwafanya kukamatwa wakiwa wanajipongeza kwa vinywaji katika baa ya Mandosi eneo la Dareda Kati.

"Ukiacha kucheleshwa kwa sababu za rushwa kwa mfanyabiashara huyo, baadhi ya mazao kama vitunguu na viazi vilivyokuwa vinasafirishwa vimeharibika," alisema huku akibainisha kuwa pamoja na watuhumiwa kufikishwa mahakamani, watawajibika kwa hasara hiyo ili liwe fundisho kwa wengine.



Askari polisi wakiuchukua mwili wa wakala wa basi la Kisbo lenye namba za usajili T 192 DBZ, linalofanya safari zake kati ya Mwanza na Dar es Salaam, Athumani Omari (38), baada ya kufariki kwa kukanyagwa na basi hilo, wakati akilirukia lilipokuwa likiondoka katika Stendi Kuu ya Mabasi mkoani Shinyanga jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Taasisi ya Mo Dewji yatoa mamilioni kuikabili kansa

**Na Enock Charles**

TAASISI ya Mo Dewji imetoa msaada wa Sh. milioni 100 kwa Tumaini la Maisha (TLM), asasi isiyo ya kiserikali inayofanya kazi na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kutoa huduma na matibabu kwa watoto wenye saratani nchini.

Msaada huo umetolewa ikiwa ni sehemu ya kujitolea kwa kila mwaka katika kuboresha ustawi wa huduma na matibabu kwa watoto wenye saratani.

Kituo cha Kitaifa cha Saratani cha Watoto kilichoko MNH ni wodi ya kwanza ya watoto wenye saratani nchini kwa mujibu wa taarifa kutoka kwa asasi hiyo. TLM ilizinduliwa na kusajiliwa Novemba 2011 nchini.

Taasisi ya Mo Dewji pia imeahidi kutoa msaada wa kila mwaka kama mchango wake kuboresha juhudi za kugharamia vifaa tiba na dawa pamoja na kusaidia programu za kliniki kuwawezesha wananchi wanaoishi katika maisha magumu kupata tumaini la maisha.

Taasisi hiyo pia imeeleza kuwa lengo lake ni kwa watoto wote wenye saratani nchini, wapate huduma bora zitakazowapa uponyaji unaofanana na nchi zilizoendelea.

Taasisi hiyo pia inalenga kuhakikisha hakuna mtoto wa Tanzania anayefariki dunia kwa saratani na kuwahimiza wananchi wote kuunga mkono juhudi za taasisi hiyo kuwasaidia wananchi wanaoishi katika mazingira magumu.

# DC atoa hadhari upandaji holela bei

**Na Mohab Dominick,** BUKOMBE

MKUU wa Wilaya ya Bukombe Mkoani Geita, Said Nkumba, amewatahadharisha wafanyabiashara kupandisha bei ya vifaa vya kutakasa mikono vinavyotumika kama kinga ya maambukizo ya virusi vya corona.

Amesema wafanyabiashara wanaotumia fursa ya ugonjwa huo kujipatia fedha kwa kupandisha bei ya vifaa hivyo kwa wananchi, watachukuliwa hatua za kisheria watakapobainika, huku akiwasihi kuendelea kuuza bei ya kawaida.

Nkumba alitoa onyo hilo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake na kusisitiza kuwa watakaokaidi agizo hilo watafungiwa huduma zao.

"Wafanyabiashara wanatakiwa kuendelea kuuza bidhaa bila kupandisha bei. wasichukulie fursa ya corona kujipatia kipato kikubwa. Niseme tu tunaendelea kutekeleza maagizo ya serikali kwa kutoa elimu kwa wananchi.

"Tumedhibiti kwa kiwango kikubwa, tumeungana na viongozi wa dini katika utoaji wa elimu hiyo. Niseme Bukombe hakuna ugonjwa wa corona.

"Tumesitisha maeneo yenye mikusanyiko kama sehemu za starehe na kumbi, ngoma za asili, minada na vyombo vya usafiri kwa abiria wote kukaa kwenye viti," alisema Nkumba.

Aliongeza kuwa kamati ya ulinzi na usalama imetembelea maeneo yote yenye mikusanyiko ikiwamo stendi ya mabasi ili kuhakikisha suala la kunawa mikono limetekelezwa inavyostahili. Mkuu huyo wa wilaya aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari ya kuepukana na maambukizi ya corona kwa kunawa mikono, salamu kwa kutoshikana mikono na kutoshiriki mikusanyiko ya watu wengi huku akiwahimiza viongozi kutoendesha ibada kwa muda mrefu.



Mafundi wa kampuni ya Simac Ltd, wakiendelea na ujenzi wa karavati katika barabara yenye urefu wa kilomita moja inayojengwa kwa kiwango cha lami kutoka Hoteli ya Kilimanjario hadi Hospitali Teule ya Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Waziri aonya visingizio corona miradi ya umeme

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amewataka makandarasi wanaotekeleza miradi ya usambazaji wa umeme vijijini, kujikinga na kuchukua tahadhari dhidi ya virusi vya corona ili kuendelea kutekeleza miradi hiyo na kuikamilisha kwa wakati kwa mujibu wa mikataba.

Dk. Kalemani alisema hayo juzi wakati akiwasha umeme katika Kituo cha Afya cha Bwina, Chato mkoani Geita. Pia aliwasha taa za barabarani zinazotumia mwanga wa jua (solar) na kuhamasisha wananchi kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo.

Alisema tishio la virusi vya corona lisirudishe nyuma juhudi za utekelezaji wa miradi ya usambazaji umeme vijijini kwa kuwa tayari mamlaka husika zimetoa miongozo ya kujikinga na kujihadhari katika maeneo mbalimbali nchini.

"Tujikinge na tuchukue tahadhari dhidi ya corona. Kazi ya kusambaza umeme vijijini lazima iendelee tena kwa kasi ya hali ya juu na miradi ikamilishwe kwa wakati uliopangwa. Cha muhimu makandarasi wafuate miongozo iliyotolewa na mamlaka husika ili kutekeleza majukumu yenu. Lazima tufanye kazi tusambaze umeme, wananchi wanataka umeme uwake," alisema.

Kalemani pia aliwasisitiza makandarasi kutotumia kisingizio cha kuwapo virusi vya corona kuchelewesha au kutokamilisha miradi ya kusambaza umeme vijijini pamoja na ujenzi wa mradi mkubwa wa kufua umeme kwa kutumia maji wa Mwalimu Nyerere katika Mto Rufiji.

Alisema mamlaka husika zimeweka wazi na kuendelea kutoa matangazo kila kona ya nchi namna bora ya kujikinga na kuchukua tahadhari dhidi ya virusi vya corona, hivyo makandarasi katika maeneo yao ya kazi wahakikishe wanasimamia na kutekeleza miongozo hiyo.

Akizindua na kuwasha taa za barabarani katika mitaa ya Chato, Dk. Kalemani alisema lengo la kuweka taa hizo ni kuongeza usalama kwa wananchi wanaotumia barabara hizo nyakati za usiku.

Dk. Kalemani pia aliwasha umeme katika kituo kipya cha afya cha Bwina wilayani hapa ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za afya wakati wote kwa wagonjwa wanaofika kutibiwa. Waziri huyo ambaye ni Mbunge wa Chato, aliwataka wananchi kulinda miundombinu ya taa hizo na kuitunza ili idumu kwa muda mrefu kwa faida yao.

Pia aliwasisitiza wananchi kuendelea kutekeleza maagizo na maelekezo yanayoendelea kutolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na wadau mbalimbali wa afya ya kujikinga na virusi vya corona, ikiwamo kunawa mikono mara kwa mara, kuepuka misongamano na mikusanyiko na kutoa taarifa pale wanapomwona mtu mwenye dalili za ugonjwa huo kama zinavyoelezwa katika matangazo.

Dk. Kalemani alikuwa akifanya ziara hiyo pasipokuwa na mikutano ya kuzungumza na wananchi, kusimama umbali mrefu kati yake na baadhi ya watu alioambatana nao, vyombo vya habari na kunawa mikono kila baada ya kufika eneo husika na kupaka kitakasa mikono ili kujikinga na corona.

# Wachumba mbaroni tuhuma za biashara dawa za kulevya

**Na Hellen Mwango**

WAKAZI wawili wanaodaiwa kuwa wachumba, wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam wakikabiliwa na mashtaka ya kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya.

Washtakiwa hao ni Josephat Mrosso na Fatuma Ally, wakazi wa Mbezi Beach, jijini Dar es Salaam.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Rashid Chaungu. Wakili wa Serikali, Elia Athanas, alidai kuwa katika shtaka la kwanza, washtakiwa hao wanajihusisha na biashara ya dawa za kulevya kwa madai kuwa Februari 28, mwaka huu, eneo la Mbezi Beach, Majani ya Chai, Kinondoni jijini Dar es Salaam walijihusisha na dawa za kulevya aina ya heroin gram 75.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa Februari 28, mwaka huu eneo la Mbezi Beach, Majani ya Chai, washtakiwa wote kwa pamoja walijihusisha na dawa za kulevya aina ya bangi gramu 617.2

Pia katika shtaka la tatu, washtakiwa hao wanadaiwa kukutwa na vitu vyenye kemikali yenye uhusiano na dawa za kulevya aina ya bangi gramu 586.2 kosa wanalodaiwa kulifanya Februari 28, mwaka huu.

Baada ya kuwasomea mashtaka, Wakili Athanas alidai upelelezi wa kesi hiyo uko katika hatua za mwisho, hivyo aliomba siku 14 ili kukamilisha jalada hilo.

Aidha, Athanas aliiomba mahakama kutowapa dhamana washtakiwa hao kwa kuwa Sheria ya Kupambana na Dawa za Kulevya inaelekeza kuwa mtu anapokutwa na dawa za kulevya zaidi ya gramu 20, hastahili kupata dhamana. Hakimu Chaungu alisema washtakiwa hao warudishwe rumande kama sheria inavyoagiza na kuahirisha kesi hiyo hadi Aprili 9, mwaka huu

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF kuweni makini ratiba lala salama

**WAKATI** Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), limesimamisha ligi zake zote ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19), ambao umesambaa sehemu mbalimbali duniani, huu ni wakati wa wasimamizi wa Ligi Kuu Bara kuandaa kwa umakini ratiba mpya.

Ratiba hiyo mpya inatakiwa itolewe kwa kuzingatia uwiano wa mechi zilizobakia za timu zote 20 zinazoshiriki ligi hiyo ya juu hapa nchini, ambayo pia hutoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Ratiba hiyo itakayokuwa na uwiano, itaondoa malalamiko kutoka kwa viongozi wa klabu na wadau wa soka hapa nchini na itatakiwa kuzingatia mazingira na jiografia ya nchi.

Licha ya kuzingatia changamoto hizo, ratiba hiyo mpya inatakiwa pia itupie 'macho' timu zenye viporo kwa sababu tayari ligi hiyo imeshaingia hatika hatua ya lala salama.

Mechi za ligi zitakapopangwa kwa kufuata weledi, itasaidia nchi kupata bingwa anayestahili na kwenda kupeperusha vema bendera ya nchi katika mashindano ya kimataifa.

Msimu kadhaa nyuma na hasa msimu uliopita tulishuhudia waliokuwa wawakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba ya jijini Dar es Salaam ikiwa na idadi kubwa ya 'viporo', jambo ambalo liliifanya timu hiyo baadaye kupangiwa mechi mfululizo.

Simba ilijikuta na jukumu la kucheza mechi kila baada ya siku moja, uamuzi ambao ulikuwa ni kinyume na kanuni za ligi hiyo, ambazo zinasema totauti ya mechi moja na nyingine ni saa 72, lakini haikuwa hivyo.

Lakini kwa kuangalia upungufu uliojitokeza msimu uliopita, na janga la corona, huu ni wakati kwa TFF na vyombo vyake kuhakikisha wanaifanyia kazi ratiba mpya itakayotolewa kwa kutosahau kuipangia timu yoyote mechi zake.

Nipashe inatoa tahadhani hii hasa kufuatia kuwapo kwa mabadiliko katika timu zinazoshuka daraja, idadi ya timu zimeongezeka, hivyo kama ratiba haitakuwa rafiki, huenda baadhi ya klabu zikaumia.

Huu ni wakati wa kuhakikisha TFF inatumia mapumziko haya kujiridhirisha na mabadiliko itakayofanya na mafanikio yatakayoonekana katika mechi chache zilizosalia, yatasaidia kufanya vema kwenye maandalizi ya msimu ujao.

Ratiba hiyo inatakiwa pia izingatie michuano ya Kombe la FA ambayo inaendelea, kwa kutoa nafasi sawa kwa timu kupumzika.


Mara kadhaa huonekana viporo kuchangia kupanga matokeo kwa baadhi ya timu kukata tamaa ya kupambana hasa kwa zile ambazo zinauhakika kwa kutoshuka daraja.

Kujifunza au kugeza kwa nchi zilizoendelea si dhambi, TFF na Bodi ya Ligi (TPLB), msisite kwenda kutafuta msaada wa upangaji wa ratiba kwa vyama vya soka vilivyoendelea, tunaamini kwa kutoa ratiba isiyokuwa na 'makandokando', itasaidia kuondoka malalamiko, lakini mwisho wa siku italinda afya za wachezaji wetu.

Hakuna siri, Ligi Kuu Bara ndiyo inayotegemewa katika kutoa wachezaji wengi wa kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars), hivyo kuwapangia ratiba rafiki kutawaepusha na majeraha yasiyo ya lazima, wakati huu bado nchi ikisubiri kujua tarehe mpya ya kuanza kwa fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), ambayo nayo imesogezwa mbele kutokana na janga la corona.

Ratiba bora pia itawasaidia wachezaji kuonyesha viwango vyao katika muda huu ambao dirisha la usajili kuelekea msimu mpya litafunguliwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Barnabas Maro

# Ama kweli fedha fedheha

**ILISEMWA** na wahenga kuwa "fedha fedheha" wakiwa na maana fedha huweza kuleta mambo ya aibu baina ya binadamu. Methali hii yaweza kutumiwa kutuonya kuhusu maovu yanayoweza kusababishwa na fedha.

Pia walisema "Fedha ilivunja nguu, milima ikalala." Maana yake fedha zina uwezo wa kuivunja milima na vilima. Methali hii yaweza kutumiwa kupigia mfano uwezo wa fedha. Mtu akiwa na fedha anaweza kufanikiwa kufanya mambo ambayo asingeweza kuyafanya wala kudhania kuyafanya.

'Uongozi' ni dhamana ya kusimamia jambo kwenye taasisi au penginepo; madaraka anayopewa mtu kusimamia au kuongoza shughuli. Hii si kazi rahisi kwani inahitaji hekima na kujitolea kwa hali na mali. Kuna wakati kiongozi hupaswa kutumia fedha zake ili kuweka mambo sawa kwa kile anachokiongoza.

Kwa hali yoyote iwayo, umwonapo mtu anayegombea nafasi yoyote ya uongozi, siasa (ubunge, udiwani au hata serikali za mitaa), michezo, hasa kandanda n.k. anagawa fedha au 'zawadi' ili achaguliwe, tambua mtu wa namna hiyo hafuati uongozi bali anafuata fedha ili ajinufaishe kwa jasho la wengine. Mtu wa namna hiyo hafai kupewa uongozi.

Janga (balaa) hili ndilo linaloisumbua Yanga na kusababisha wadhamini wao, GSM, kuchukizwa na kuandika barua ya kusimamisha misaada isiyo kwenye mkataba. Baadhi ya viongozi wanailalamikia GSM kwa madai kuwa inaingilia mambo ya uongozi! Wanataka fedha zinazotolewa na GSM wakabidhiwe viongozi ili wazigawe kwa wachezaji, badala ya GSM kuzigawa!

GSM wanasema fedha wanazotoa hazimo kwenye mkataba hivyo wanatoa kwa mapenzi yao. Kwamba ingawa wataendelea kuwa na Yanga, hawatatoa fedha zozote nje ya mkataba wao na klabu. Ni yale yale ya "Fedha ilivunja nguu milima ikalala."

Sasa matawi ya Yanga yanatofautiana na baadhi ya viongozi wanaotaka GSM iwe inakabidhi fedha zake kwa uongozi wa klabu. Viongozi wa aina hiyo ni wale niliowataja huko juu kwa hugombea uongozi ili kujinufaisha badala ya klabu. Viongozi wa aina hii wanapaswa kuogopwa wa sana kwani kilichowapeleka Yanga si kuiletea maendeleo, bali Yanga ndio iwaendeleze katika mambo yao!

Tabia hii haikuanza leo kwani imekuwa mazoea ya baadhi ya viongozi wanaotaka kujinufaisha kwa fedha za wadhamini badala ya kuinufaisha klabu. Huko nyuma watu waliojitolea kusaidia maendeleo ya Yanga walijitoa walipogundua badala ya kuinufaisha klabu, waliwanufaisha viongozi waroho!

Kama mtu anajitolea kuwapa wachezaji hela ili wafanye vizuri, kwa nini alazimishwe kukabidhi hela hizo kwa viongozi wa klabu? Viongozi wanaodai kuwa anayewapa wachezaji fedha anakwenda kinyume cha klabu ilhali jambo hilo halimo kwenye mkataba, wana maana gani? Enyi mliogombea uongozi kwa lengo la kujinufaisha, bora mjiuzulu mapema kabla ya kufukuzwa. Wafadhili wengi waliotaka kuibeba Yanga kwa hali na mali walijitoa baada ya kugundua fedha zao zinaliwa na viongozi walioingia klabuni kujinufaisha badala ya kuinufaisha klabu na wachezaji. Wakigundulika, wafukuzwe!

Viongozi wanaotaka GSM iwape wao fedha badala ya kuziwasilisha kwa wachezaji ambao ndiwo wanaostahiki, wao ndio waondoke Yanga ili wakaanzishe klabu yao.

Kuna wakati Reginald Abraham Mengi (Mungu amrehemu) alitaka kuifanya Yanga iwe ya kimataifa na kujitegemea yenyewe. Kwa maana hiyo alimtoa mchumi wake (naye Mungu amrehemu) kufungua ofisi klabuni Yanga ili afanye maandalizi ya kuiendeleza Yanga. Baadhi ya viongozi walioona wamenyimwa fursa ya kutafuna fedha za klabu, wakawaweka wale waitwao 'makomandoo' kumvuruga Mengi pale alipoandaa mkutano wa Yanga na kumtukana. Akaona hakuna sababu kuwasaidia watu wasiokuwa na shukrani, akaondokea palepale Uwanja wa Uhuru.

Huo ni mfano mmoja tu bila kuwataja wengi waliojitolea kwa hali na mali kuisaidia Yanga lakini viongozi walaji wakatumia fursa hiyo kujinufaisha badala ya kuinufaisha klabu na wachezaji! Mwaka jana kuna kiongozi fulani alithubutu kuliambia gazeti moja la michezo kuwa "kupiga pesa" si vibaya ila usizidishe! Kwa lugha ya mitaani, 'kupiga pesa' maana yake ni kula hela. Ndivyo baadhi ya viongozi walaji wanavyotaka kufanya kwenye klabu ya Yanga! HAWAFAI, HAWAFAI, HAWAFAI! Mwenye masikio asikie.

Kama kuna viongozi walioingia Yanga kwa lengo la kula hela, bora wajiondoe wenyewe wakatafute sehemu za kula magendo lakini watambue siku watakapokamatwa, watakuwa wageni rasmi kule Segerea wakisubiri mbivu na mbichi kwenye Mahakama ya Kisutu jijini Dar es Salaam.

"Epuka maovu nayo yakwepuke." Unapoyaepuka mambo mabaya huwezi kufikwa na ubaya wowote. Methali hii yatufunza kujitenga na mambo mabaya yanayoweza kutuletea madhara.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

# Mbaroni kwa tuhuma utakatishaji bil. 75/-

**Na Hellen Mwango,**

WATUMISHI sita wa Kampuni ya Simu ya Viettel Tanzania, akiwamo Mkurugenzi Mtendaji wa Halotel, Son Nguyen (46), wamefikishwa mahakamani kwa tuhuma za uhujumu uchumi ikiwamo kuisababishia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) hasara na kutakatisha zaidi ya Sh. bilioni 75.

Vigogo hao walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu Monica Mbogo akisaidiana na Wakili wa Serikali, Turumanya Majigo.

Mbogo aliwataja washtakiwa wengine kuwa ni, Nguyen Minh (40) na Vu Tiep, wote ni Mameneja wa Halotel, Ha Than (39) ambaye Mtaalamu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) Halotel, Mkurugenzi wa Fedha wa kampuni hiyo, Nguyen Cong na kampuni ya Viettel.

Mbogo alidai kuwa kati ya Juni 8, 2017 na Machi 26, mwaka huu eneo la Mikocheni, Kinondoni, jijini Dar es Salaam, washtakiwa hao waliongoza genge la uhalifu ili kujipatia faida.

Alidai kuwa kati ya Juni 8, 2017 na Machi 26, mwaka huu, eneo la Mikocheni na maeneo mengine ya nchi, kwa pamoja walitumia masafa ya redio bila kupata kibali kutoka TCRA.

Pia alidai kati ya Julai 7, 2016 na Machi 26, mwaka huu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Vietnam, kwa pamoja walitengeneza mfumo ambao ulitumia huduma za mawasiliano zinazojulikana kama Virtual Private Network (VPN) kinyume cha taratibu.

Katika shitaka la nne, inadaiwa washitakiwa hao walikwepa kulipa kodi kwa TCRA kwa kutumia mitambo ya mawasiliano yaliyounganisha Viettel Tanzania na Vietnam kinyume cha sheria.

Ilidaiwa kuwa Juni 8,2017 na Machi 26, mwaka huu eneo la shtaka la nne kwa kutumia masafa ya redio bila kupata kibali cha TCRA, waliisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni 75.

Pia ilidaiwa kuwa kati ya Julai 7, 2016 na Machi 26, mwaka huu kwa kutumia mitambo ya VPN waliisababishia TCRA hasara ya Sh bilioni 3.03.

Katika shitaka la saba, washtakiwa wote wanadaiwa kutakatisha Sh. bilioni 3.03 wakati wakijua fedha hizo ni zao la makosa ya kuongoza genge la uhalifu.

Shtaka lingine, Kampuni ya Viettel Tanzania inadaiwa kati ya Julai 7, 2016 na Machi 26, mwaka huu, ilitakatisha Sh. bilioni 3.03 na mashitaka ya tisa na 10, washtakiwa wote wanadaiwa kutakatisha Sh bilioni 75 wakati wakijua fedha hizo ni zao la uhalifu.

Washtakiwa hawakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi na upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika, uliomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu Simba alisema kwa kuwa mahakama yake haina mamlaka ya kusikiliza kesi, washtakiwa wapelekwe rumande mpaka Aprili 9, mwaka huu, itakapotajwa.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mafunzo ya Amali Zanzibar, Abdulla Abdulla, akizungumza katika uzinduzi wa mradi wa visima virefu vya maji safi katika shule za msingi na sekondari visiwani humo jana, kwa ufadhili wa asasi ya Time To Help na shule za Feza. Wa (tatu kulia) ni Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Simai Mohamed Said. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Asasi yasaidia visima shule Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

ASASI ya Time To Help kwa kushirikiana na shule ya Feza na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, imezindua mradi wa visima virefu vya maji katika shule za msingi na sekondari visiwani Zanzibar.

Mradi huo ambao utatekelezwa mwaka huu, utahusisha uchimbaji wa visima 20 shuleni na utagharimu takribani Sh. milioni 150.

Uzinduzi wa mradi huo ulifanywa na Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohamed Said, kwenye mkutano na waandishi wa habari makao ya wizara ya elimu na kuhudhuriwa na viongozi waandamizi wa wizara hiyo.

Wengine waliohudhuria ni wawakilishi kutoka Wizara ya Utumishi wa Umma Zanzibar, Mwenyekiti wa taasisi ya SABIL ambao ndio wamiliki wa shule za Feza Zanzibar, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Feza Zanzibar, Ali Nungu, na Mweyekiti wa Asasi ya Time To Help, Ramadhani Praph.

Praph alisema katika kipindi cha miaka miwili iliyopita taasisi hizi mbili (Time To Help na Feza) zimeshachimba visima 30 Zanzibar (Unguja na Pemba) na kwamba kwa mwaka huu wa 2020 wameweka malengo ya kuchimba visima 20 shuleni.

Alisema katika visima hivyo 20, mpaka sasa maeneo 14 yameshatengwa kwa ajili ya uchimbaji na maeneo sita bado. Alisema malengo yao ya visima 20 mpaka mwezi huu, visima vinne tayari vimeshachimbwa na kuzinduliwa katika skuli za Muanda na Wete Sekondari, Pujini na Mizingani Msingi na Sekondari.

Pia alisema visima vitatu uchimbaji wake unaendelea ambavyo ni Mgambo na Kijumbani Msingi na Sekondari na Skuli ya Msingi Sebleni.

Alisema lengo la kujenga visima shuleni ni kusaidia harakati za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika juhudi za kuboresha elimu kwa kupeleka maji safi na salama shuleni ambako kutapunguza usumbufu na kupoteza muda kwa wanafunzi katika kutafuta maji.

Kutokana na msaada huo, alisema muda mwingi utatumiwa na wanafunzi kujifunza zaidi, hivyo kuongeza ufaulu wa masomo na kwamba wanafunzi wakiwa na maji safi na salama shuleni, watajikinga na maradhi mbalimbali.

Naibu Waziri Simai alishukuru Time To Help na shule za Feza kwa msaada huo wa upelekaji wa vyanzo vya maji shuleni.

Simai alisema vyanzo hivi vya maji vitasaidia kutatua kero ya upatikanaji wa maji shuleni pamoja na wananchi wanaozizunguka shule hizo hivyo kuleta tija katika kuboresha elimu na afya ya wanafunzi na wananchi.

# Matatani kusafirisha wahamiaji haramu

**Na Manuel Kaminyoge,** SONGWE

JESHI la Uhamiaji mkoani Songwe linawashikilia wakazi watatu wa Wilaya ya Ileje kwa tuhuma za kusafirisha watu sita wanaodaiwa wahamiaji haramu ambao walivushwa kinyemela kupitia mpaka wa Tanzania na Malawi.

Kamanda wa Uhamiaji Mkoa wa Songwe, Wilfred Marwa, alisema jana ofisini kwake kuwa wahamiaji hao walikamatwa na kuzuiwa na wananchi wa kata ya Bupigu wilaya ya Ileje wakiwa kwenye usafiri wa pikipiki.

Alisema mpaka wa Tanzania na Malawi kwa zaidi ya kilometa 150 uko wazi, hivyo wamekuwa wakitoa elimu kwa wananchi na kuwapa mbinu za kuwatambua wahamiaji haramu, ndiyo maana wamefanikisha kuwakamata watu hao.

Kamanda Marwa aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari mbalimbali kwa wageni wanaoingia kwenye maeneo yao hasa katika Wilaya za Momba na Ileje ambazo ziko mipakani huku akitahadharisha kuwa wananchi wa wilaya hizo wako hatarini zaidi hasa katika kipindi hiki ambacho nchi inapambana na ugonjwa wa corona.

"Niwatake wananchi wa wilaya za Momba na Ileje wasikubali kuwapokea raia wa kigeni na wachukue tahadhari juu ya ugonjwa wa corona," alisema.

Mmoja wa wananchi wa kata ya Bupigu na shuhuda wa ukamataji wa wahamiaji hao haramu, Ubatizo Songa, alisema elimu zinatolewa na Uhamiaji kila siku lakini wanajiuliza wenzao wanaokiuka sheria za nchi wana mpango gani.

Aidha, Songa alisema ukamataji huo ni wa pili kutokea kwenye kata hiyo kwa kuwa hivi karibuni walifanya hivyo na kwamba hawaruhusu raia yeyote mgeni kupita bila kibali au kujitambulisha.

Songa alisema wananchi wa eneo hilo wanapohisi kuwa mtu huyo si raia wa Tanzania, wanalazimika kutoa taarifa Uhamiaji na Polisi .

Katika kuwakamata watu hao juzi, alisema waliwatambua madereva wa pikipiki, maarufu kama bodaboda na walipowasimamisha mara ya kwanza, waligoma kusimama na kwenda kukamatiwa kijiji Cha mbele ambako kila dereva pikipiki aliwabeba wahamiaji hao haramu wawili.

Mkuu wa Wilaya ya Ileje, Joseph Mkude, aliwatahadharisha wananchi wanaofanya kazi ya kuwavusha na kuwasafirisha wahamiaji haramu na kuwataka waache kwa kuwa serikali haitawaacha salama.

Pia aliwataka wananchi kuendelea kuwadhibiti na kuwakamata watu ambao wanawatilia shaka kwa kuwa kufanya hivyo ni faida kwa jamii ya wana Ileje, mkoa na taifa kwa ujumla.

## Kampuni yatoa msaada Tabora

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

KAMPUNI ya Tumbaku ya Alliance One Tanzania (AOTTL), imeukabidhi uongozi wa Mkoa wa Tabora vifaa mbalimbali vikiwamo vya ujenzi vyenye thamani ya Sh. milioni 23.9.

Msaada huo ulikabidhiwa jana na Mkurugenzi wa Uzalishaji wa Kampuni hiyo, David Mayunga, kwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, katika hafla iliyofanyika ofisini kwake mjini Tabora.

Mayunga alivitaja vifaa vilivyotolewa kuwa ni mabati 270, saruji mifuko 300 na nondo 320.

Alisema msaada huo ni kwa ajili ya ujenzi wa mabweni na vyoo katika Wilaya za Tabora na Uyui ili kuwasaidia watoto wa kike.

Mayunga alisema Wilaya ya Tabora imepewa mifuko 200 ya saruji na nondo 240, vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 8.6.

Alisema msaada huo ni kwa ajili ya ujenzi wa mabweni katika shule za Sekondari Itojanda na Ndevelwa, zote za Manispaa ya Tabora.

Mayunga alisema kwa upande wa Wilaya ya Uyui, wamekabidhi mabati 250, mifuko 100 ya saruji na nondo 80 kwa ajili ya kuunga mkono ujenzi wa mabweni ya watoto wa kike katika Sekondari ya Idete na kumalizia majengo ya shule mpya ya Nsimbo.

Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Mwanri, aliwataka wakuu wa wilaya zote zilizopata msaada huo, kuhakikisha vifaa hivyo vinatumika kwa malengo ya kutoa mazingira mazuri kwa watoto wa kike kupata elimu.

Alionya kuwa hatasita kuchukua hatua kwa watendaji wote waliopewa vifaa ambao watavitumia kwa maslahi binafsi.

Mkuu wa Wilaya ya Tabora, Komanya Kitwala, aliishukuru Kampuni ya Alliance One kwa msaada huo ambao utawasaidia kuongeza kampeni yake ya kujenga mabweni kwenye shule mbalimbali ili kuwakinga watoto wa kike dhidi ya mimba.

Alisema hatua hiyo ni muhimu katika kukabiliana na watoto kutembea umbali mrefu kwenda shuleni na huku njiani wakikutana na vishwawishi.

Mkuu wa Wilaya ya Uyui, Gift Msuya, alisema msaada waliopata, utasaidia kumalizia mabweni ya wasichana katika Shule ya Idete ambayo walikuwa wameshaanza kujenga chini ya Kampeni ya Nishike Mkono kuwasaidia watoto wa kike wapate elimu.

# Kinondoni yapuliza dawa kuzuia corona

**Na Mwandishi Wetu**

HALMASHAURI ya Manispa ya Kinondoni kwa kushirikiana na wataalamu wa afya wa Mkoa wa Dar es Salaam, imepuliza dawa katika vituo vya mabasi yaendayo haraka na vituo vya daladala, ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kudhibiti maambukizi ya virusi vya corona.

Upuliziaji wa dawa pia umefanyika katika maeneo mbalimbali yakiwamo makazi ya wananchi, maeneo ya kutolea huduma mbalimbali, yakiwamo masoko, makanisa na msikiti.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mstahiki Meya wa Halmashauri hiyo, Benjamini Sitta, alisema hatua hiyo imechukuliwa ili kuua wadudu wanaosababisha maambukizo ya virusi hivyo na wamepanga kupuliza dawa kwenye maeneo yote ya halmashauri hiyo.

Meya Sitta alisema ugonjwa huo ambao umekuwa tishio kubwa duniani na halmashauri imejipanga kikamilifu katika kuukabili usisambae kwa kusambaza wataalamu wa kupulizia dawa hiyo kwenye kata zote za halmashauri hiyo.

"Kwa ujumla, tunashiriki ipasavyo katika kupambana na maambukizo ya virusi hivi, kwa pamoja tunaunganisha nguvu kutoka kwenye ngazi ya mkoa, Kinondoni ni halmashauri mojawapo ambayo imeanza zoezi hili kwenye maeneo yote na leo tumeanzia Kata ya Msasani ambayo ndiyo kuna watalii wengi," alisema.

Mratibu wa Malaria Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Ford Chisongela, alisema mkoa unashirikiana na halmashauri kuhakikisha unatokomeza ugonjwa huo unaosababishwa na virusi hivyo hatari.

Alisema kuwa katika kuongeza nguvu ya kupulizia dawa hiyo, mkoa umeamua kutumia magari ya Zimamoto pamoja na yale ya Jeshi la Polisi Kikosi cha Kutuliza ghasia (FFU) kwa kuwa yana uwezo mkubwa wa kufanya kazi kwa haraka na hivyo kuwatoa hofu wananchi wasishtuke pindi watakapoyaona mitaani.



Mkurugenzi wa Teknohama na Uendeshaji wa Benki ya Posta (TPB), Jema Msuya (kushoto), akikabidhi mifuko 200 ya saruji yenye thamani ya Sh. milioni 3.7 kwa Mbunge wa CCM, Viti Maalum wa Mkoa wa Rukwa, Bupe Mwakang'ata, kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa mkoani humo, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# RC aviweka sawa vikosi vita corona

**Na Mwandishi Wetu,** SONGWE

MKUU wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali Nicodemus Mwangela, amesema maandalizi ya kukabiliana na ugonjwa wa homa ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona kwa mkoa wake yako vizuri.

Hata hivyo, amezielekeza halmashauri za wilaya kukamilisha baadhi ya upungufu uliobainika katika kudhibiti kuenea kwa virusi hivyo.

Aliyasema hayo jana akiwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa mara baada ya kukamilisha ukaguzi wa utayari wa kukabiliana na ugonjwa huo katika Halmashauri za Mbozi, Ileje na Mji wa Tunduma.

Alisema watalaamu wa afya ambao watawahudumia wagonjwa wa corona endapo watatokea mkoani Songwe, tayari wana mafunzo na uelewa wa majukumu yao huku vituo vilivyoteuliwa kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa na washukiwa, vikizingatia maelekezo ya Wizara ya Afya. Brigedia Jenerali Mwangela aliongeza kuwa amebaini baadhi ya vituo vya kutolea huduma kwa wagonjwa na washukiwa wa corona vina upungufu kadhaa ikiwamo uhaba wa maji, umeme na baadhi ya vifaa tiba na kinga, hivyo akaziagiza halmashauri husika kukamilisha mahitaji hayo haraka.

Kiongozi huyo wa mkoa ameendelea kutoa elimu ya kujikinga na virusi hivyo kwa wasafiri, madereva na wafanyakazi wengine wa mabasi katika maeneo mbalimbali huku akiwasisitiza kuchukua hatua za tahadhari kwa kunawa mikono na kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima.

"Nimetembelea vituo vinne ambavyo vimetengwa kwa ajili ya kuwahudumia wagonjwa na washukiwa wa virusi vya ugonjwa wa corona endapo watatokea na nimeaona tatizo kubwa ni shida ya maji na umeme.

"Nimeagiza na kuwapa siku moja Wakuu wa Wilaya ya Mbozi na Ileje waimalize matatizo hayo," alisema.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, George Salala, aliwaagiza wamiliki wa vyombo vya usafiri kuhakikisha hawajazi abiria kuliko uwezo wa gari kwa kuwa kufanya hivyo ni kutengeneza mkusanyiko usio wa lazima na kuonya kuwa hatua kali zitachukuliwa kwa watakokaidi.

Pia, alitoa angalizo kwa abiria kutokubali kupanda mabasi au usafiri wa aina hiyo endapo watakuta hali hiyo, watawachukulia hatua za kisheria.

Alisema wamiliki wa mabasi wanapaswa kuweka maji ya kunawa yenye dawa katika mabasi yao ili kuwakinga madereva wao na abiria dhidi ya ugonjwa huo.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Dk. Hamad Nyembea, alisema mpaka sasa, maandalizi ya utayari wa kukabiliana na ugonjwa wa Corona kwa mkoa huo yamefikia asilimia 50.

Dk. Nyembea alibainisha kuwa kutokana na agizo la serikali la kuwaweka karantini siku 14 watu wote wanaotoka nchi zenye maambukizo ya corona, hadi sasa wamewaweka karantini watu sita waliotumia mpaka wa Tunduma wakitokea Afrika Kusini.





Mkuu wa wilaya ya Arusha, Gabriel Daqarro akiongea na wananchi katika stendi ya mabasi makubwa ya mkoa wa Arusha jana, wakati akizindua rasmi zoezi la kupulizia dawa kinga ya maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona kwenye magari yaendayo mikoani. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Msikiti wajenga kitega uchumi kujinasua na kuomba misaada

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

WAUMINI wa Msikiti wa Masjid Taqwa mkoani Manyara, wamejikwamua kiuchumi baada ya kujenga vyumba vya biashara ili viwasaidie kulipia maji na umeme.

Hayo yalisemwa jana mjini hapa na Sheikh wa Mkoa wa Manyara, Mohamed Kadidi, wakati akizungumza na Nipashe.

Alisema wao wanaamini kufanya kazi ni sehemu ya ibada, hivyo wanahimiza suala la uchumi kuanzia mtu mmoja mmoja na kuanzisha biashara za kuingizia kipato.

"Tumeamua kuwekeza kwenye ujenzi wa vyumba vya biashara ili kupunguza shida ya kulipia maji na umeme, ambayo tunayatumia na itusaidie kuendesha taasisi," alisema Sheikh Kadidi. Alisema watu wengi hawatambui kuwa wana fursa ya kuanzisha biashara yoyote na kujipatia kipato na kuachana na kuomba msaada kila siku.

"Unaomba kila kitu mpaka watu wakikuona wanakukimbia maana wanajua ukiwafuata unawaomba. Hiyo si nzuri tujikwamue kwa kuanzisha biashara hata kama ndogo," alisema.

Aidha, alisema walikubaliana wajenge vyumba 50 na kwa sasa wameanza na vyumba 13 kwa awamu ya kwanza ambayo inaisha Mei, mwaka huu.

Kadidi aliwashauri waumini wa misikiti mingine kuiga mfano wa msikiti huo ambao umeanzisha miradi ya ujenzi kwa manufaa ya waumini wake. Alisema iwapo taasisi zao zitaanzisha miradi ya maendeleo, itaisadia kupiga hatua zaidi kwa ustawi wa maendeleo ya taasisi za dini.

# Wataka sera jumuishi maendeleo jinsia

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

SERIKALI imeshauriwa kutambua haki na changamoto za jamii za pembezoni na kuziingiza katika sera mpya ya maendeleo ya wanawake na jinsia, ambayo inatarajiwa kufanyiwa maboresho mwaka huu.

Wito huo ulitolewa jana katika kikao cha mashirika yasiyo ya kiserikali 20 ya Mkoa wa Arusha katika kikao cha kupitia Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2002 na kutoa mapendekezo katika sera mpya ambayo inatarajiwa kutolewa na serikali. Mratibu wa Jinsia katika Mtandao wa Mashirika ya Wafugaji, Wawindaji wa Asili na Waokota Matunda (Pingos Forum), Nailejileji Tipap, akizungumza katika kikao hicho, alisema kuna baadhi ya maeneo jamii za pembezoni zimetengwa. Tipap alisema kutokana na baadhi ya upungufu katika sera hiyo ya mwaka 2002, ndiyo maana wamekutana kama mashirika kuanza kutoa maoni na mapendekezo katika sera mpya ambayo inaandaliwa.

Meneja Mipango wa Baraza la Wanawake (PWC), Alais Melau, alisema sera mpya ya maendeleo ya wanawake na jinsia ni muhimu kujumuisha maoni ya wadau wote. Alisema kuna mambo ambayo yanapaswa kuingizwa katika sera mpya, ikiwepo masuala ya umiliki ardhi kwa wanawake, uwezeshwaji kiuchumi wanawake wa pembezoni na masuala ya ushiriki katika vyombo za uamuzi. Katika kikao hicho pia mashirika hayo yalitaka kutambuliwa utamaduni wa jamii za pembezoni, changamoto za kielimu na kimazingira katika kuhakikisha wanapata utetezi katika sera hiyo.

# DC apongeza utii wananchi

**Na Cynthia Mwilolezi,**
SIMANJIRO

MKUU wa Wilaya ya Simanjiro Mkoani Manyara, Zephania Chaula amewapongeza wakazi wa wilaya hiyo kwa kufuata maagizo ya serikali ya kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima katika kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona.

Chaula aliyasema hayo jana wakati akielezea mwitikio wa wananchi katika kuhakikisha wanatekeleza maelekezo ya serikali juu ya kupambana na maambukizo ya virusi vya ugonjwa huo.

Alisema wananchi wa wilaya hiyo wanaendelea kufanya shughuli zao za kiuchumi, huku wakitii maagizo yaliyotolewa na serikali ikiwemo kunawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka kila baada ya kumaliza kufanya jambo lolote lile.

Chaula alisema kwenye shughuli zozote za kiuchumi na nyumbani, ameagiza maji yatengwe ili watu wanawe mikono na agizo hilo limetekelezwa na wananchi wa eneo husika.

"Hata kwenye lango la kuingia ndani ya ukuta unaozunguka migodi ya madini ya Tanzanite mji mdogo wa Mirerani, kumewekwa maji ili kila anayetoka na kuingia anawe mikono kwa sabuni na maji chirizi," alisema Chaula.

Alisema amekagua maeneo ya migodini na kukuta wachimbaji wameitikia agizo hilo kwa kuweka madumu ya maji kwenye milango ya migodi yao na wafanyakazi wao wananawa kila wakati wa kazi.

"Hata kwenye minada na maeneo mengine ya wilaya ya Simanjiro wananchi wameitikia kwa kufuata maelekezo yaliyotolewa na serikali yao na nawapongeza kwa hilo," alisema Chaula.

Alisema wananchi wa wilaya hiyo wameahidi kuendelea kufuata maagizo yaliyotolewa na Rais John Magufuli, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu juu ya kujikinga na corona.

Mkazi wa Kata ya Terrat, John Loishiye, alimpongeza mkuu huyo wa wilaya kwa kutofunga minada kama baadhi ya maeneo mengine kwa kuwa wafugaji wanaitegemea kiuchumi.

Loishiye alisema maisha ya wafugaji yanategemea minada, hivyo watatekeleza maagizo ya serikali katika kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima wakiwa minadani.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti (wa pili kushoto), Mkurugenzi wa Mji wa Babati, Fortunatus Fwema (kushoto) na viongozi wa CCM wa mkoa huo, wakikagua ujenzi wa jengo la CCM la mkoa huo, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wamiliki wa gesti, kambi za utalii watakiwa kuunga mkono vita corona

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

SERIKALI imewataka wamiliki wa nyumba za kulala wageni na kambi za muda za kulaza watalii mkoani Kilimanjaro, kutojiweka pembeni katika mapambano dhidi ya homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona, badala yake wajitokeze kuiunga mkono.

Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Kippi Waroba, alitoa rai hiyo jana mjini hapa, alipokutana na kufanya mazungumzo na wafanyabiashara wanaomiliki vitegauchumi hivyo.

"Jamani tumewaita hapa kuwaomba mwongeze nguvu katika mapambano dhidi ya ugonjwa huu. Tushirikiane na serikali kuhakikisha ugonjwa huu hatari wa corona ambao sasa ni janga la dunia, unadhibitiwa ili usiingie katika mkoa wetu wa Kilimanjaro," alisisitiza Warioba

Warioba amezitaka menejimenti za hoteli zote katika Wilaya ya Moshi kuyafanyia kazi mafunzo maalum yaliyotolewa na wataalam wa afya mkoani Kilimanjaro ili wawe na uelewa sahihi juu ya maambukizi na dalili za ugonjwa wa Corona.

Kwa mujibu wa Warioba, hivi sasa serikali mkoani Kilimanjaro inatekeleza agizo la Rais John Magufuli la kuhakikisha wageni wote wanaoingia nchini wanawekwa katika karantini ya siku 14 kabla ya kuruhusiwa kuchangamana na watu ili kuendelea na shughuli zao.

Mwanzoni mwa wiki hii, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, aliwaagiza wakuu wa mikoa, makatibu tawala wa mikoa na wakuu wa wilaya kubainisha hoteli za gharama ndogo ili wanaoingia nchini kutoka nchi zenye maambukizo ya virusi vya corona, wamudu na kukaa karantini kwa siku 14.

Ummy alilazimika kutoa maelekezo hayo baada kuibuka malalamiko ya baadhi ya wageni kuwa wanapelekwa kwenye hoteli zenye bei kubwa hali inayosababisha kushindwa kumudu gharama.

Machi 24, mwaka huu, kupitia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Twitter, Ummy alisema: "Tumepokea hii changamoto ya sehemu zilizobainishwa kwa ajili ya siku 14 za wasafiri waliotoka nchi zilizoathirika zaidi na virusi vya corona kukaa.

Nawaelekeza ma-RC (Wakuu wa Mikoa) na ma-RAS wa mikoa yote (makatibu tawala wa mikoa) kubainisha hoteli na sehemu ambazo wasafiri wengi watamudu gharama."

# Shule yatikiswa ujauzito wanafunzi

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

SHULE ya Sekondari ya Somsom iliyoko Moshi mkoani Kilimanjaro, imeendelea kutikiswa na mimba za utotoni, baada ya jana Diwani wa Kibosho Magharibi (CCM), Deo Mushi, kuibua mazito akidai kuwa wanafunzi wengine wawili zaidi wamebainika kupata ujauzito.

Jana, Mushi alieleza masikitiko yake kuhusu hali hiyo, zikiwa zimepita takriban wiki tatu tangu mwanafunzi mwingine wa kidato cha nne wa shule hiyo ajifungue mtoto akiwa chooni na kisha kumtupa mwanae chooni akiwa nyumbani kwao.

"Hao waliogundulika tena kupata ujauzito ni wanafunzi wa kidato cha pili, watoto kuendelea kupata mimba ni kwa sababu bodi ya shule haijaonyesha uwezo wake katika kuchukua hatua za kinidhamu na kuacha suala hili likielea,"alisema

Alipoulizwa kuhusu tatizo hilo, Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Juma Tukosa, alisema yeye si msemaji wa jambo hilo badala yake aulizwe Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba.

Siku chache zilizopita, diwani huyo alinukuliwa akidai kuwa uhusiano mbovu kati ya uongozi wa kata na shule hiyo yanaweza kuongeza tatizo zaidi.

"Nasisitiza kuwa kumekuwapo na mahusiano (uhusiano) mabaya (mbaya) kati ya uongozi wa shule na Ofisi ya Mtendaji wa Kata ambapo bodi ya shule nayo haitoi ushirikiano mzuri katika kuendesha shuguli za pamoja za hapo shuleni ikiwamo kusimamia nidhamu na mahitaji ya wanafunzi.

"Jitihada za Mtendaji wa Kata (Elisha Moses) kuiweka shule kwenye msimamo wa kiserikali. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selamani Jafo, alishatoa maagizo kuwa walimu wakuu waliodumu miaka mitano shule moja wahamishwe maana kuna kuishi kwa mazoea.

"Ni muhimu sasa bodi ya shule ikatafakari umuhimu wa wazazi tuanze kusaidiana katika kulea watoto pamoja na ombi letu la kujenga hosteli ya wasichana ndio inahitaji kuwekewa mkazo kwa sasa," aliongeza.

Aidha, Mwanaharakati Vicky Massawe, anayepambana na vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto, kupitia mradi wa nguvu ya pamoja unaoendeshwa na Shirika la Kilimanjaro Women Information Exchange and Community Organization (Kwieco) kwa ufadhili na Women Tanzania Fund (WFT), alisema kuna haja serikali ikatafuta ufumbuzi wa kudumu wa haraka katika shule hiyo.

Kwa mujibu wa mwanaharakati huyo, kumpa mimba mwanafunzi ni kosa la jinai, chini ya kifungu cha 60A cha Sheria ya Elimu, Sura 353, kama kilivyofanyiwa marejeo na kifungu cha 22 cha Sheria, namba 2 ya mwaka 2016.

Kifungu cha tatu (3) cha sheria hiyo kinaeleza kuwa mtu yeyote atakayepatikana na hatia ya kumpa mimba mwanafunzi wa shule ya msingi au sekondari atatumikia kifungo cha miaka 30 jela.

Sheria hiyo hiyo, kifungu cha tano (5) inamtaka kila mkuu wa shule kuandaa taarifa ya kila robo mwaka ya matukio ya wanafunzi walioolewa au kupewa ujauzito na kuiwakilisha kwa kamishna wa elimu.

# DED aonya ujenzi holela

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

MKURUNGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, Ndaki Muhuli, ameonya kuwa ujenzi holela na usio na vibali unaoendelea katika maeneo ya kandokando ya barabara kuu ya Sanya Juu/ West Kilimanjaro, utasababisha hasara kubwa kwa wananchi wanaokaidi kufuata sheria za ujenzi.

Muhuli alitoa onyo hilo jana baada ya kupokea malalamiko ya baadhi ya wakazi wa wilaya hiyo, waliohoji ukimya wa serikali katika kuzuia ujenzi unaoendelea wa majengo ya biashara kwenye maeneo yasiyoruhusiwa kisheria.

"Suala la kujenga bila vibali halipaswi kuvumiliwa, naonya tena wanaoendelea kufanya ujenzi waache mara moja ili kuepuka bomoabomoa isiyo ya lazima. Niwashauri wananchi wa Siha kwamba ni vyema kufuata sheria na taratibu za ujenzi wa makazi yao ili kuepuka bomoabomoa,"alisisitiza

"Nikiri kwanza kwamba nilipata barua za malalamiko kuhusu ujenzi holela kutoka kwa baadhi ya wananchi kwamba barabara inayoelekea majengo ya zamani ya halmashauri yetu, kuna watu wamejenga vibanda vya biashara na kuifanya kupitika kwa shida," alisema.

Kutokana na tatizo hilo, mkurugenzi huyo ameahidi kutuma wataalamu wa halmashauri hiyo kufanya ukaguzi katika majengo yanayolalamikiwa na kisha kuwasilisha ripoti hiyo ofisini kwake.

"Watakwenda wataalamu katika maeneo yote yanayolalamikiwa na watoa elimu kwa wananchi ili waweze kuendeleza ujenzi unaozingatia utaratibu, tunataka mji wa Sanya Juu uwe wa kisasa zaidi na mwonekano mzuri,"aliema Mhuli

Akizungumzia malalamiko hayo, Diwani wa Sanya Juu ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Juma Jani (CCM), alisema kama hakutachukuliwa hatua za haraka ni wazi kuwa vilio vinavyotokana na makali ya bomoabomoa na machozi ya waathirika, vitajenga sababu ya kugawana lawama kati yao na serikali.

"Inawezekana ni kweli katika gharama ya kutafuta maendeleo, lazima wachache waumie, ingawa pia kuna uwezekano wa kuchukua tahadhari mapema kupunguza makali kwa kutumia njia rafiki," alisema Jani.



# Taasisi ya Mkapa yaajiri wataalamu afya 2,000

**Na Augusta Njoji,** DODOMA MJINI

JUMLA ya wataalamu wa afya 2,181 wameajiriwa kupitia Taasisi ya Benjamin Mkapa (BMF) ndani ya miaka 14, imeelezwa.

Taasisi hiyo pia inatarajiwa kukamilisha usaili wa wataalamu wa afya 80 wiki ijayo ambao watapelekwa kwenye Hospitali za Rufani nchini.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Dk. Ellen Mkondya-Senkoro, wataalam hao walioajiriwa, wanatoa huduma katika hospitali na vituo vya tiba nchini hususani vya serikali na taasisi za kidini. "Tunashukuru serikali kwa ushirikiano endelevu na taasisi yetu kwa miaka 14 tangu ilipoanzishwa mwaka 2006 hadi Desemba 2019, tumewezesha kutoa ajira 2,181," alisema.

Alibainisha kuwa uwezeshaji huo umetokana na ufadhili mbalimbali kutoka Mfuko wa Dunia wa Kupambana na Ukimwi, Malaria na Kifua Kikuu, Shirika la Irish Aid, Serikali ya Norway na Mfuko wa Abbott.

Alisema taasisi hiyo imekuwa sehemu ya mikakati ya kitaifa ya kuimarisha huduma za Ukimwi, kifua kikuu na malaria.

"Kuna watumishi 307 wa halmashauri 68 kwenye mikoa 11 wamepangiwa vituo vyao vya kazi na wametakiwa kuwa wameripoti Machi 27 mwaka huu na hawa ni wa fani mbalimbali," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema taasisi hiyo inaamini ubunifu, ufanisi na matokeo makubwa ya haraka na kuahidi kuwa itaendelea kushirikiana na serikali.

"Naomba serikali iendelee na ushirikiano wa aina hii na asasi zisizo za kiraia ikiwamo yetu katika kuleta maendeleo yanayoonekana dhahiri na yenye kumnufaisha mwananchi hasa aliyeko kijijini,"alishauri.

Aliahidi kuwa taasisi hiyo itakuwa mstari wa mbele kupambana na ugonjwa wa corona kupitia miradi yao ambayo imeweka wataalamu wa afya vituoni na wahudumu wa afya ngazi ya jamii.

Akizungumza kuhusu ajira hizo, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, aliishukuru taasisi hiyo kwa kuimarisha mifumo ya sekta ya afya nchini.

Alitoa wito kwa asasi zingine zisizo za serikali kusaidia kuimarisha huduma za afya ikiwamo kutoa elimu ya namna ya kupambana na ugonjwa wa corona badala ya kujikita kwenye semina zisizo na tija.

## DC aonya wananchi mlipuko wa corona

**Na Renatha Msungu,** DODOMA MJINI

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, amewataka wakazi wa Dodoma kuzingatia ushauri wa wataalamu wa afya katika kujikinga dhidi ya ugonjwa wa homa ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona.

Katambi alitoa rai hiyo jana alipopokea msaada chupa 3,600 za vitakasa mikono kutoka Kampuni ya Shoppers Plaza kwa ajili ya taasisi mbalimbali.

Alisema vitakasa mikono hivyo vimesambazwa katika taasisi mbalimbali vikiwamo ofisi za vyombo vya habari na kuwataka wananchi kutopuuza ushauri unaotolewa ili kutopata maambukizo ya ndani kwa ndani.

"Tunashukuru kwa msaada huu, mmesaidia serikali kukabiliana na ugonjwa huu, tunataka kuona kila mmoja anatumia kabla ya kuingia ofisini," alisema.

Katambi alitoa wito kwa watengenezaji wengine wa vitakasa mikono, kuiga mfano wa taasisi hiyo ili kusaidia nchi kuukabili ugonjwa huo.

"Wananchi wangu fuateni kanuni zinazotolewa ili kujiweka salama na familia zenu, pia muepuke misongamano kama ilivyotangazwa na serikali," alisihi.

Alisema kinachotakiwa kwa sasa ni kila mmoja kuchukua hatua dhidi ya mwenzie ili kila mwananchi awe salama.

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Shoppers Plaza, Ashley Fermandes, alisema wataendelea kutoa msaada huo kusaidia serikali katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

"Tutahakikisha hakuna litakaloshindikana na kwa kushirikiana na serikali kupambana na ugonjwa huu ambao sasa unasumbua dunia,"aliahidi.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa mtaro wa kupitisha maji ya mvua katika Barabara ya Martin Luther, eneo la Swaswa, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Chamwino waomba kujengewa daraja

**Na Augusta Njoji,** CHAMWINO

WANANCHI wa Kijiji cha Manda wilayani Chamwino mkoani Dodoma, wameiomba serikali kufanya matengenezo katika daraja lililokatika na kukata mawasiliano kati ya kijiji hicho na Jiji la Dodoma.

Wamesema kukatika kwa daraja hilo kumesababisha gharama za usafiri kupanda kutoka Sh. 6,000 hadi Sh.30,000.

Akizungumza na Nipashe, Diwani wa Manda, Fredrick Mandyamba, alisema kijiji hicho kipo umbali wa zaidi ya kilometa 100 kutoka jijini humo na daraja hilo lilisombwa na mvua tangu Novemba mwaka jana.

"Yaani si rahisi kufika mjini, kuna tope na maji yamejaa, tunasafiri kwa tabu, gharama za usafiri zimepanda maana tunalazimika kutumia pikipiki kupita njia nyingine hadi kijiji kingine ndiyo tunapata usafiri wa basi," alisema.

Alisema kukatika kwa daraja hilo pia kumeongeza bei ya bidhaa, hivyo kuwafanya wananchi kushindwa kuzimudu.

"Pia, eneo hili ng'ambo huko kuna shule mbili tofauti, ipo ya Sekondari Maila na Magharibi kuna Shule ya Msingi Manda, sasa korongo likijaa watoto kabla shule hazijafungwa walikuwa hawawezi kwenda shule, wakati corona inakuja, sisi watoto walishaacha kwenda shule zamani tu," alisema.


Kiongozi huyo wa kisiasa aliomba serikali isaidie kwa haraka kutatua matatizo yanayowakumba wananchi kutokana na kukatika kwa daraja hilo.

Matei Mapunda, ambaye gari lake limenasa kwenye tope la daraja hilo, alisema: "Hatuwezi kumfikishia mtu mzigo wake kwa wakati, kama alitakiwa kufikishiwa baada ya siku moja, inatuchukua wiki nzima barabarani, tunaomba serikali iliangalie hili."

Alisema wanaelekea msimu wa mavuno na mahitaji yao yote wanategemea kupata Dodoma mjini, lakini hadi sasa hawaelewi watasafirishaje.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Kambona Matonya, alisema baada ya daraja kukatika, alifika Ofisi ya Halmashauri na kuongea na Mkurugenzi Desemba 22 mwaka jana.

"Desemba 23 mwaka jana, nilifika ofisi ya Mkuu wa Mkoa nikapeleka nakala niliyowasilisha ofisi ya wilaya, baada ya hapo waliahidi kufika kuona uharibifu na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura)





Makamu Mwenyekiti wa chama cha ADA-TADEA, Juma Ali Khatib (kushoto), akimuwekea dawa ya kuosha mikono (sanitizer), Msajili Msaidizi Idara ya Usajili wa Vyama vya Siasa, Sixty Nyahoza, aliyefika kufanya uhakiki katika ofisi za chama hicho, zilizopo eneo la Mombasa, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali yasifu mchango wadau elimu

**Na Rahma Suleiman,** UNGUJA

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali, imesema inathamini michango inayotolewa na taasisi zisizo za kiserikali katika kuchangia maendeleo ya sekta ya elimu nchini.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Simai Mohammed Said, aliyasema hayo alipozindua mradi wa ujenzi uchimbaji wa visima unaotekelezwa na Jumuiya ya Time to Help ya Tanzania Bara kupitia Shule ya Feza kwa Shule 14 kati ya 20 za Unguja na Pemba.

Alisema uchimbaji wa visima hivyo utasaidia kwa kiasi kikubwa serikali katika kutatua matatizo katika upatikanaji wa maji kwenye baadhi ya shule na hata vijiji vya karibu na shule hizo, kufaidika na huduma hiyo.

Alisema katika mwaka wa fedha 2019/2020, Baraza la Wawakilishi ilipitisha Sh. bilioni 178 katika kutimiza majukumu ya wizara, lakini wameona umuhimu wa kutafuta fursa mbalimbali ambazo zitaiendeleza sekta hiyo.

"Wizara yetu ni kubwa kwani tuna shule zaidi ya 206 za sekondari na nyingine tunajenga, hivyo wale wanaoungana na sisi katika kutusaidia, tutaendelea kuwaunga mkono kwa hali na mali," alisisitiza.

Aliahidi serikali itaendelea kuipa ushirikiano taasisi hiyo katika kutekeleza mradi huo na miradi mingine ili kufikia malengo waliyoyakusudia na kuleta tija kwa wanafunzi wa Zanzibar.

Sambamba na hayo, aliipongeza taasisi hiyo kwa mambo mengi inayoyofanya katika kuwasaidia wananchi wa Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kaimu Katibu Mkuu ambaye pia Naibu Katibu Mkuu Utawala na Uendeshaji, Abdullah Mzee Abdullah, alisema zaidi ya wanafunzi 12,000 na wananchi walio karibu na maeneo ya hayo, watanufaika na mradi huo katika kupata huduma ya maji safi na salama.

Alisema shule hizo ni tisa za Unguja; Muanda, Mgambo, Chunga, Dimani, Uzi Ngambwa, Kandwi, Paje, Mtende na Sebleni na kwa upande wa Pemba ni Wete, Pindua, Kizimbani, Kijumbani na Mohammed Juma Pindua.

Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Praph Ramadhan, alisema imejikita katika kutoa huduma mbalimbali za kijamii ikiwamo maji katika sekta ya elimu ili wanafunzi wasome katika mazingira mazuri na safi.

Aliishauri wizara kufanya tathimini kila mwaka katika visima vinavyochimbwa ili kujua maendeleo yake na kuendana na utoaji wa huduma bora ya maji safi na salama sambamba na kuelimisha wanafunzi katika shule hizo ili kuvitunza visima hivyo vitumike kwa muda mrefu.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Feza, Ali Nungu, aliahidi visima hivyo vitakamilika ndani ya mwaka huu ili wanafunzi wapate huduma hiyo muhimu.

Zaidi ya Sh. milioni 150 zinatarajiwa kutumika katika uchimbaji wa visima hivyo na uwekaji wa matanki ya maji katika skuli hizo.

# Kiwanda chafungwa kisa 'sanitizer' zisizo na ubora

**Na Rahma Suleiman,** UNGUJA

BODI ya Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar (ZFDA), imekifungia kiwanda cha kutengeneza dawa za kutakasa mikono (sanitizers) cha OIL CAM, baada ya kubainika dawa hizo kutokuwa za kiwango kinachohitajika na kutosajiliwa kisheria.

Hatua ya kukifungia kiwanda hicho kilichoko Kiembesamaki, imechukuliwa baada ya kutolewa kwa taarifa kutoka kwa wasamaria wema, waliobaini kuwapo kiwanda hicho huku mamlaka za serikali zikiwa hazijakihalalisha.

Akitoa taarifa hiyo, Mkuu wa Kitengo cha Vipodozi cha ZFDA, Salim Hamad Kassim, alisema kiwanda hicho kimekuwa kikitengeneza vitakasa mikono kwa ajili ya kujikinga na maambukizo ya corona bila idhini ya serikali na bidhaa zake hizo hazina kiwango kinachohitajika.

Alisema kiwanda hicho kimebainika kutengeneza bidhaa hizo kwa kiwango duni na kuweka alama feki kwamba bidhaa hizo zinatoka nje ya nchi.

Mkaguzi wa Ubora na Usalama na Ufanisi wa Dawa Sokoni, Nassir Salum Buheti, alisema watawaagiza wenye maduka kutoziuza bidhaa za kiwanda hicho na kutoa elimu kwa wananchi ili kununua bidhaa ambazo zinakuwa na ubora.

Alisema bodi yao itafanya msako zaidi katika kipindi hiki cha mlipuko wa maradhi ya corona ili kuhakikisha bidhaa zinazouzwa zinakuwa na kiwango na zimethibitishwa.

Alisema kumekuwapo na wajasiriamali ambao wanatengeneza vitakasa mikono duni, wakitumia fursa ya ukubwa wa soko la bidhaa hizo kutokana na maambukizo ya corona

# Tadea wakoshwa uhakiki wa chama

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha ADA Tadea, Juma Ali Khatib, amesema wameridhishwa na uhakiki wa ofisi za chama chao, hatua inayowapa nafasi zaidi ya kuendelea na maandalizi ya uchaguzi mkuu.

Amesema kufanikisha uhakiki wa chama ni hatua muhimu kukiwezesha kuwa na sifa za kuwa chama cha siasa na kufanya kazi zake kwa mujibu wa sheria.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya chama hicho kufanyiwa uhakiki na Msajili wa Vyama vya Siasa nchini.

"Uongozi wa chama cha ADA Tadea tumefurahishwa kwa kufanikisha uhakiki wa usajili wa vyama vya siasa na hivyo kutupa nafasi ya hatua nyingine ya kufanya shughuli zetu kihalali pamoja na maandalizi ya uchaguzi mkuu wa Zanzibar," alisema.

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini iko katika mchakato wa kuhakiki vyama vya siasa ikiwamo kuangalia sifa za vyama hivyo na uhalali wake ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka huu.

Msajili Msaidizi Idara ya Usajili wa Vyama, Sixty Nyahoza, alisema ofisi yao tangu kuanza kwa uhakiki mjini Unguja, imefanikiwa kuvikagua vyama vitatu ambavyo ni CCM, CUF na ADA Tadea, na wamevikuta vimejiandaa vizuri kufanikisha kazi hiyo.

Alisema wakati wakifanya ukaguzi huo, ADA Tadea kiliwapatia vielelezo muhimu vya usajili huo ikiwamo orodha ya wanachama wao, ofisi wanazozitumia, cheti cha usajili, Bodi ya Wadhamini na mali za ofisi.

Alisema hali ya chama hicho haiko vibaya, akibainisha kuwa baadhi ya vyama wamebaini kuwapo kwa matatizo mbalimbali yakiwamo ya ukosefu wa ofisi na vimekuwa vikitumia nyumba za kuishi na familia za baadhi ya wanachama.

Alisema matatizo mengine waliyobaini ni namna ya vyama vinavyoshindwa kuweka kumbukumbu za wanachama katika mifumo ya kompyuta.



**LULU DIVA HUJUI MAPENZI KIKOHOZI?** Soma UK.15

JUMAMOSI MACHI 28, 2020

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



# Nani kumuoa Hamisa Mobetto?

BASI SAWA

# Machozi usitoe chozi, ndio dunia

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Hussein Machozi, amekasirishwa na kitedo cha watu kumzushia kifo kila mara, akisema wanatamani afe kweli ili wafurahi.

Hussein Machozi amesikitishwa na taarifa hizo na akaeleza yeye ni mzima wa afya na yuko salama.

Amewataka watu kumwambia kosa lake alilowahi kufanya basi ili awaombe watu msamaha na si kumzika huku akiwa hai.

"Kha jamani mbona mnaniua namna hii, hata kama hamnipendi si hivi asee mimi nipo salama tena nina afya tele, msinifanyie hivi jamani kwani niliwakoseaga nini mniambie basi niwaombe msamaha maana mara ya pili sasa mnaniua, ama mnataka nidedi kweli", ameandika Hussein Machozi.



# Ebo! Ebitoke corona haina utani ujue

MCHEKESHAJI Ebitoke amewaacha mashabiki wake midomo wazi baada ua kusema ana muda wa wiki moja anahisi kama ana dalili za ugonjwa wa Corona.

Akizungumza hivi karibuni, Ebitoke amesema tangu ugonjwa huo umeanza amechukua tahadhari za kupunguza misongamano na kushinda ndani, ila haelewi dalili hizo zimetokana na nini.

"Tahadhari za Corona ni kujikinga kwa kuvaa mask, kuepuka mikusanyiko ya watu na kushinda nyumbani, hapa nilipo nahisi nina dalili za Corona kwa asilimia maana nina shida mwilini, kwa kuwa nimeshakuwa na dalili hizi nitachukua hatua ya kupima ili nijue kama ninao au sina" ameeleza Ebitoke.





# Chuchu Hans hilo unalo tu

MWIGIZAJI nyota nchini Chuchu Hansy, amesema kuwa na uhusiano na mtu maafuru kumemtumbukia nyongo na hatua hiyo anaijutia.

Chuchu ana uhusiano wa kimapenzi na mwigizaji mwenzake, Vicent Kigosi "Ray" ambao sasa wana mtoto mmoja.

Akizungumza kupitia Planet Bongo ya East Africa Radio, amesema kama mwanamke anahitaji tuzo ya kipekee kwani kuwa na mtu maarufu anapitia changamoto nyingi.

"Sijawahi kukosana na Baba Jayden, mimi ni mwanamke mwenye historia kwake na hatoweza kutokea mwingine, ila kitu nachojutia kwake ni uhusiano wangu kuwa wazi na 'kudeti'na mtu maarufu" amesema Chuchu Hansy.

Alitaja changamoto anazopitia ni kuwa na wivu pale wanawake kumkumbatia, kufuatwa na wanawake wazuri au kum-kiss".

## INSTA-TWITTER





**Kila** mcheza kamari ana siri yake ya kipekee katika kupata ushindi, kamwe hazifanani-**Irene Paul.**



**Hivi** mwanaume ukitaka kutoka kwenda sehemu, unaomba ruhusu kwa mwenzi wako au unatoa taarifa?-**Ray Kigosi.**



# Lulu Diva hujui mapenzi kikohozi?

LULU Diva ameibuka na jipya wiki hii, baada ya kumpa sharti zito mchekeshaji Idris Sultan, kama anataka kurudiana na Wema Sepetu.

Akizungumza na EATV, Lulu Diva amesema Idris na Wema, walikuwa wanapendana ma angefurahi kuwaona wamerudiana, lakini safari hii mapenzi yao yawe ya siri.

"Idris na Wema wanawasiliana na wanaongea vizuri, siku zote mnapoachana sio lazima muwe maadui na mapenzi ya kweli huwa hayaishagi, wale watu walikuwa wanapendana sana, nitafurahia kuona wamerudiana ila kwa hali ya utofauti na ile ya awali" amesema Lulu Diva.

Akaongeza "Kama watarudiana tena au akiwa na uhusiano na mwanamke yeyote yule isingependa kumuona mapenzi yake yakiwa hadharani kama mwanzo, nataka mapenzi yao yawe siri."

## UNASEMAAA...

# Nedy mambo mengine magumu kuyasema



MSANII wa muziki wa kizazi kipya, Nedy Music, amejilipua kwa kusema huwa na kawaida ya kupika, kuosha vyombo hata kumfulia nguo mpenzi wake.

Nedy Music amesema, anafanya hivyo kutokana na thamani anayompa mwanamke wake kwa kuwa anamfanyia vitu vingi na yeye binafsi hachagui kazi.

"Huwa nafanya vitu vingi kwa ajili yake, mimi ni mwanamume ambaye hata kwa mwanamke wangu naweza kumfulia nguo zake bila kujali chochote, thamani yangu kwake ni kubwa kwahiyo hata nguo za ndani inawezekana kabisa kumfulia" amesema Nedy Music.

Aidha ameendelea kusema "Sidhani kama kumfulia mpenzi wako ni ishu kubwa, kama utaiangalia kiubinadamu na kiuwanaume"



# Wolper hii sasa kali

MSANII wa filamu za Bongo muvi, Jacqueline Wolper, ameanika vigezo ambavyo mwanamume anayetaka kupata naye mtoto anatakiwa kuwa navyo.

Akizungumza kupitia video fupi 'aliyoposti' katika akaunti yake ya a Instagram, ambapo amevitaja vigezo vya mwanaume huyo.

"Nataka niwe na mtoto, unajua umri unakwenda lakini nani atakuwa ndiyo baba, mimi nataka asiwe tajiri, awe mchapakazi ajue kazi na asichague kazi, hata nikimwambia leo tunaenda Kariakoo shimoni kuna dili ya nyanya zimetoka tukanunue, tuuze tupate pesa awe tayari kwa kifupi asiwe bishoo," amesema.

Aidha akataja vigezo vingine kuwa awe ana hofu ya Mungu, asiwe anavuta sigara wala unga, kilevi chochote ruksa, asiwe staa wa kabila lolote wala dini yoyote. Awe msafi muda wote asiwe na mtoto, umri ni miaka 30 na kuendelea, urefu ufupi uzuri siyo tatizo, muhimu vigezo uwe navyo hajalishi uwe mbaya au la, maana sipendi wanaume wazuri.

Hivi sasa Jacqueline Wolper anatajwa kuwa kwenye mahusiano na msanii wa HipHop hapa nchini

## INSTA-TWITTER



**Nawapenda** sana wageni wangu ila kwa sasa sipokei mgeni yoyote nyumbani kwangu. Wageni wengine wabishi mno ukiwaambia osha mikono wabishi. Nikiwaambia pakeni 'hand sanitizer' pia wabishi, wakati wanajua janga kubwa linalotuzunguka sasa. Siwahitaji tena tutaonana inshaallah CORONA ikiisha-**Shamsa Ford.**



**Unapataje** furaha baada ya kujua umevuruga ndoa ya mtu? Acha kuwapenda waume za watu, maana hujui wamepitia nini mpaka kuijenga ndoa yao. Mahusiano yenye furaha kutoka moyoni ni yako na mumeo, siyo mume wa mtu. Mungu hapendi Jamani punguzeni kudanga kwa waume za watu. Mchana mwema-**Emmanuel Mbasha.**



**Kujiamini** ni sehemu ya maisha lakini kujiaminisha kwamba unajiamini inaitaji ujasiri zaidi-**Wema Sepetu.**

Kuumbe!



# Nani kumuoa Hamisa Mobetto?

BAADA ya muda mrefu kupita tangu atangaze yupo singo, mwanamitindo na mwimbaji, Hamisa Mobeto amekiri na kuwa yupo kwenye lindi la mahaba na mwanaume mmoja.

Hata hivyo, uhusiano huo umeibua gumzo baada ya mrembo huyo kuficha jina la mwanaume huyo, licha ya kuweka wazi wana mpango wa kufunga ndoa.

Hamisa Mobeto ameeleza kupitia insta story ya mtandao wa Instagram, kwamba kutokana na utamu wa penzi hilo wiki ijaayo inawezekana wakafunga ndoa.

Hata hivyo baadhi ya mashabiki wake wamedai msanii huyo hana mpango huo na anachokifanya kama njia ya kujiongezea umaarufu.

Hamisa ambaye ni mama wa mtoto mmoja wa mwanamuziki Diamond Platnumz, amekuwa na uhusiano wa kimapenzi na mastaa tofauti, lakini hawafiki mbali na kuachana.

Msanii huyo alitoa muda kwa mashabiki zake kumuuliza maswali yoyote, kisha yeye kutoa majibu. Moja kati ya maswali aliyoulizwa yalikuwa ni bado yupo singo, shemeji yeo ni nani, na harusi yake ni lini?

"Sijarudiana na EX wangu na sipo singo, nipo kwenye mahusiano sasa hivi, ila nina shemeji yenu mzuri, siku ya ndoa mtamuona inshaalah na harusi wiki ijayo".

Pia kupitia mitandao ya kijamii kuna stori ambazo zinaeleza kuwa huenda Hamisa Mobetto na Alikiba wamefikia hoteli moja huko visiwani Zanzibar, baada ya ramani "location" zao kusoma zipo sehemu moja hali ambayo inafanya watu kuwaza vitu tofauti.

Mashabiki wake wanasubiri kuona atakayekuwa mume wa Hamisa, lakini wengi wanahoji nani atakuwa tayari kufunga pingu na mlimbwende huyo?

# Majoka, madebe waliyowachengua matozi



CHAKACHAKA

Na Adam Fungamwango

ILIKUWA ni katikati ya miaka ya '80 na mwanzoni mwa '90, pamoja na kuwa kulikuwa na ushabiki mkubwa na muziki wa dansi, lakini kilizuka kizazi kipya cha wanamuziki na mashabiki wake ambao walikuwa na muziki wao tofauti.

Kulizuka mapinduzi na muziki fulani wa disco, ambapo waliokuwa wakichipukia wakati huo waliiita 'kuruka majoka' au 'kucheza madebe'. Na hii ilitokana na aina ya muziki uliokuwa ukipigwa ambao ulikuwa tofauti na muziki wa dansi wa kawaida.

Badala yake lilikuwa ni disco lilikuwa na mchanganyiko wa muziki wa Kimarekani ambao ni Wamarekani weusi na Kiafrika.

Mchanganyiko huo ulileta ladha fulani na muziki wa disco, kwela, pop na jive, hivyo kuvutia vijana wengi ambao wakati huo waliitwa 'machekibobu' au 'mabitozi' kwa sasa wanaitwa 'matozi'.

Wasichana na watoto nao walikuwa hawashikiki kwa aina hiyo ya muziki iliyokuwa ikichengua kila mahali nchini kwenye kona za nchi nzima, pamoja na masherehe mbalimbali.

Vijana wa wakati huo walikuwa wakienda 'kucheza ndebe' kwenye kumbi maarufu wakati huo kama Mbowe, YMCA, Ushirika maarufu kama Margot, Silversands, Rungwe, Msasani Mbech, Kunduchi Beach na nyingine nyingi.

Hizi ndizo ngoma zilizokuwa zikitamba wakati huo na kuwafanya vijana wa wakati huo kutoshikika.

**YEKEYEKE-MORY KANTE**

Sidhani kama kuna kijana wa miaka ya mwishoni mwa '80 haijui ngoma hii.

Yekeyeke ndiyo ngoma maarufu zaidi ilikuwa ikichezwa na vijana na watoto wa miaka hiyo kwenye sherehe mbalimbali za kijamii, wakishindana.

Ngoma hii iliyokuwa na aina fulani na mapigo ya harakaharaka ilitoka mwaka 1987, ingawa wengi walikuwa hawamjui hata mtunzi na mwimbaji na ngoma hiyo.

Mory Kante, raia wa Guinea, ndiye mtunzi na mwimbaji wa wimbo huo uliokuwa si maarufu nchini tu, bali hata dunia nzima na kumpatia umaarufu, pesa na tuzo nyingi.

**SANGOMA-YVONNE CHAKACHAKA**

Ngoma hii nayo ilitoka mwaka 1987. Mwanamuziki wa kike aliyekuwa maarufu sana wakati huo kwa kutoka na vibao mbalimbali. Moja ya ngoma zake zilizotesa kwenye kumbi za disco na kwenye sherehe zilizowafanya watu wapagawe ni 'Sangoma' ambao ulizidi kumuweka kwenye chati.

**SWEET MAMA-PAT SHANGE**

Pat Shange ni mmoja wa wanamuziki kutoka Afrika Kusini aliyewachengua vijana wengi katikati ya miaka ya '80 hadi mwanzoni '90 kutokana na ngoma zake kali, pamoja na aina yake ya uvaaji na kunyoaji wa nywele zake akiziweka mafuta ya 'karikiti' yaliyokuwa yakitumiwa sana na akinadada wakati huo.

Moja ya ngoma zake ambazo zilikuwa maarufu mno nchini Tanzania ni 'Sweet Mama' ulikuwa kwenye albam yake ya 'Cassavova' ambao haukukosekana kwenye sherehe zozote za kijamii au kwenye madisco, mwishoni mwa miaka ya '80.

NYOSHI

PAT SHANGE

PAMELA NKUTHA

**MELODY-PAMELA NKUTHA**

Sauti ya kilio cha mtoto mchanga, pamoja na baadhi ya maneno yaliyotakwa kwa lugha moja ya huko Afrika Kusini, Wabongo wakaweka tafsiri yao wanaoijua wao ya Kiswahili wakiimba 'Uchungu wa mwana aujua mzazi,' uliufanya wimbo huo kuwa maarufu sana nchini, ukiimbwa na kupendwa zaidi na watoto na wanawake. 'Melody' ni moja kati ya ngoma zilizotisha mno kipindi hicho kwenye madisco na mitaani, mwanzoni mwa miaka ya '90.

Mtunzi na mwimbaji Pamela Nkutha mwanamama wa Kisauzi, hakuwa maarufu sana Bongo kama wimbo wake jinsi ulivyopendwa.

**JABULANI-PJ POWERS**

Ni wimbo maarufu sana miaka ya mwishoni mwa miaka ha '80 na mwanzoni mwa miaka ya '90, ukichezwa kila kona ya nchi.

Mwanamama Msauzi Penelope Jane Dunlop maarufu kama PJ Powers, ndiye mtunzi na mwimbaji wa ngoma hiyo, lakini hakuwa na umaarufu hapa Bongo, zaidi ya wimbo wake ambao mitaani kila mmoja utamsikia 'Eeee ieee ieee Jabulani.'

## IMETOKEA

# Aliwa na mamba akitoroka kizuizi cha corona



MWANAMUME mmoja nchini Rwanda ambaye alikiuka amri ya kizuizi cha nyumbani, ameuawa na mamba wakati alipokwenda mtoni kuvua samaki.

Kwa mujibu wa Meya wa Wilaya ya Kamonyi kusini mwa Rwanda, Alice Kayitesi, amesema tukio hilo lilitokea siku ya Jumatano asubuhi katika mto Nyabarongo.

"Alikiuka sheria ya kukaa nyumbani, alikuwa ni miongoni mwa watu wachache ambao hawaonyeshi ushirikiano katika sheria hii ya kukaa nyumbani ili kuzuia kusambaa kwa coronavirus ," alisema Kayitesi.

Serikali ya Rwanda iliweka amri ya kukaa nyumbani kuanzia siku ya Jumapili kutokana na kuendelea kuongezeka kwa kasi wagonjwa wa Covid-19.

Rwanda imethibitisha kuwa na wagonjwa 40, idadi hiyo ikiwa ni ya juu zaidi kuliko mataifa mengine ya Afrika Mashariki.

Kufungwa kwa shughuli za kiuchumi katika nchi hiyo kumwewaathiri watu wengi wenye kipato cha chini.

Serikali imesema kuwa itawasaidia wale wanaohangaika wakati wa hatua kali za kudhibiti maambukizi.

Polisi wamesambazwa katika maeneo mbalimbali ili kuhakikisha watu wanatekeleza amri hiyo kwa ajili ya kudhibiti maambukizi ya virusi vya corona.

Wafanyakazi muhimu, kama madaktari na wauguzi, wafanyakazi wa maduka ya jumla na waandishi wa habari, wanaruhusiwa kutoka nyumbani.

Kila baada ya kilomita 8 kuna vituo vya ukaguzi vya polisi.






## HIYARI YANGU

# Hata iwe limbwata, mapenzi hayaingiliwi

**Na Adam Fungamwango**

DHANA, hisia na uamuzi wa haraka ni kitu kibaya sana. Binadamu anatakiwa kuwa na muda wa kutafakari chochote anachoona, kuambiwa au kusikia kabla ya kutoa uamuzi.

Haraka yoyote inaweza kutoa uamuzi ambao siyo sahihi.

Jamaa mmoja alikuwa anaendesha gari akielekea mjini, anakutana na mwanzake aliyekuwa akitoka mjini kwenda nje ya mji. Yule aliyetoka mjini akashusha kioo na kumwambia mwenzake 'pundaaa'.

Kwa haraka, mwenzake anajua amemtukana, anamjibu 'punda mwenyewee'.

Kwa hasira akaongeza spidi ya gari na mita kadhaa baadaye akakutaka na kundi la punda barabarani, hakuwa na uwezo wa kufunga breki ghafla akawaparamia na kupata ajali mbaya.

Akiwa hospitali alimkumbuka yule jamaa na kugundua hakuwa anamtukana ila alimtaarufu kuwa mbele kuna punda. Kuna mifano mingi juu ya hili.

Kwenye mapenzi nako, kuna watu wanaodhani kuwa baadhi ya wanaume wamepewa limbwata na wake zao, hivyo wanatawaliwa.

Hii iko kwenye filamu iitwayo 'Hiyari Yangu', iliyochezwa na wasanii wengi, lakini maarufu ni Simon Mwapagata, Suleiman Barafu, Wellu Sengo, Muhogo Mchungu na wengineo.

Mwapagata na mkewe Wellu wanaonekana kuishi maisha ambayo ni tofauti na ilivyozoeleka.

Mume anapika chakula, anafua nguo na kufanya kazi zote za ndani, huku mkewe akiwa ametulia tuli.

Hali hiyo inamkera mno kaka wa Mwapagata, aitwaye Barafu ambaye anamkanya ndugu yake asiwe bwege. Hata hivyo yote hayo hayakusaidia, jamaa aliendelea na kazi zote za nyumbani, huku mke akiwa na kazi ya kupeleka watoto shule na kuwarudisha, lakini anaporejea anatulia tu nyumbani huku akichati na simu.

Hali ilipozidi kuwa mbaya, Barafu akaamua kuondoka nyumbani kwa mdogo wake kwani hakuweza kuvumilia hali ile. Akakimbilia kwa baba yake mdogo, Muhogo Mchungu na kumueleza kuwa mdogo wake amepewa limbwata na mkewe, kwani imefikia wakati sasa anakuna hadi nazi, mkewe akiwa amekaa tu.

Muhogo anaamua kufunga safari hadi kwa mtoto wa ndugu yake na kukuta yale yale aliyosimuliwa.

Pamoja na kumuweka chini mkewe akiwa hayupo, lakini Mwapagata hakusikia, aliendelea na kazi zake kama mtoto wa kike.

Alipoondoka wenyewe walicheka na kukumbushana kuwa bado siku tatu tu. Wellu, mke wa Mwapagata anaitisha kikao cha wanandugu wote, lakini wa kiume baadhi walisusa, kutokana na walichokiona. Kwenye kikao hicho Wellu alifafanua kuwa mumewe aliamua kufanya kazi zile kwa hiari yake kwa muda wa mwezi mmoja ambao yuko likizo ili kuangalia uzito na kazi za akinamama.

Akasema walikuwa wanabishana na mumewe kwa kuwa kuna wakati mke analalamika kuwa anachoka, hivyo akasema atakapopata likizo atakuwa akifanya kazi zote za ndani ili aone kama zinachokesha kweli au la.

Mwapagata likiri hilo na kusema kuwa kesho akaanza kazi ofisini na kazi za ndani zitaendelea kwa mkewe kama kawaida na hali ile haikuwa kama wengi walivyotafsiri kuwa amelishwa limbwata. Wengi walishangaa na wambea wakabaki midomo wazi.



CORONA YAKINUKISHA

# Idris Elba, Card B wavurugana hadharani

WASANII nyota wa Marekani, Mugizaji Idris Elba na rapa Card B wameingia katika mgogoro mzito kiasi ambacho sasa wanashambuliana.

Tofauti za wasanii hao inatokana na kauli ya Card B mapema wiki hii, akisema kuna baadhi ya mastaa wanapewa pesa ili wajitangaze wana virusi vya Covid 19

Kutokana na kauli hiyo, Elba ameibuka na kuita kauli hiyo ni ya kijinga na kwamba Card B hajitambui.

Kupitia InstaLive nyota huyo wa filamu ya 'Hobbs & Show' alifunguka kuwa tetesi hizo hazina maana yoyote, wazo hili kwamba mtu kama mimi naweza kulipwa kusema nina ugonjwa, ni jambo ambalo halina maana, Huu ni Ujinga," amesema

Akaongeza "Watu wanataka kueneza utadhani kama ni habari. Huu ni ujinga … na njia ya haraka ya kuwafanya watu wapate maambukizi"

CardiB bila kutaja jina la staa yoyote alihoji kuhusu mastaa wanaojitangaza kupata corona kuwa wote wanadai hawana dalili zozote sasa ilikuwaje wakaenda kupima?

Wakati huo huo, rapa Meek Mill amekwenda mbali na kuibua mambo mapya, baada ya kudai aliumwa ugonjwa kama wa Corona mwishoni mwa mwaka jana.

Akitumia mtandao wa Twitter kutoa taarifa hiyo Meek Mill amesema, hakuwahi kuumwa kama vile, pia hata madaktari walishindwa kuutambua ni ugonjwa gani unaomsumbua na kwa wazee ni hatari zaidi hawawezi kukabiliana nao.

"Niliumwa kama hivi mwezi Disemba karibia na sikukuu ya Christmas, nilikuwa na mafua yenye dalili za ugonjwa kama huu ambapo nilipoteza kilo 15, sikuwahi kuumwa kama vile na  sikuweza kufanya chochote, madaktari walishindwa kujua nini tatizo na kila siku nasema mtu mzee hataweza kukabiliana na ugonjwa huu"  ameandika Meek Mill.

# Kelvin Hart, Eniko kuongeza mtoto wa pili




MWIGIZAJI wa marekani, Kelvin Hart na mke wake Eniko wanatarajia kupata mtoto wao wa pili hivi karibuni.

Wanandoa hao kwa sasa wana mtoto wa miaka miwili.

Eniko ameweka wazi wiki hii kupitia ukurasa wake wa Instagram baada ya kuposti picha akiwa amevaa gauni linaloonesha tumbo lake na kuandika

"Mtoto #2 ndani ya siku chache na wote tunahesabu Baraka zetu na siwezi kuelezea furaha yetu,"



## Unachokisema Hilda wengine hawakielewi

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Nollywood, Hilda Dokubo, amewataka baadhi ya wachungaji wanaojitangaza wana nguvu za miujiza kwenda hospitali kuwasaidia wagonjwa wa vorona.

Hilda amesema wachungaji wa aina hiyo duniani kote ambao wanaamini kuwa na nguvu hizo wafanye kazi ya kusaidia waathirika wa ugonjwa huo katika kipindi hiki kigumu.

"Wachungaji wote ambao tunaamini wana nguvu za miujiza, wanaweza kwenda hospitali kuwaombea wagonjwa wa corona na kuwarudisha virusi sehemu vilivyotoka," amesema Hilda.

## Wengi waomboleza kifo cha Manu Dibango

MASHABIKI wa muziki barani Afrika, wanaendelea kuomboleza kifo cha mkongwe, Manu Dibango, ambaye aliyefariki dunia wiki iliyopita kwa ugonjwa wa Covid 19.

Dibango ambaye alianza kujulikana mwaka 1972 kutokana kibao chake 'Soul Makossa' maziko yake yatakuwa ya kifamilia.

Mwanamuziki huyo mahiri kutumia chombo cha Saxophon au maarufu kama mdomo wa bata, amefariki akiwa na umri wa miaka 86.





## Uche Jombo unafahamu peni inakosea?

MWIGIZAJi Uche Jombo, amekasirishwa na timu ya habari ya Rais Buhari akisema wana uwezo mdogo wa kuandika taarifa.

Uche aliandika katika ukurasa wake wa twitter kuwa waandishi hao wanafanya makosa mengi katika taarifa yao kiasi ambacho huamini kama watu hao wapo ofisi ya kiongozi huyo.

"Timu yote ya habari ya Rais Buhari, wanatakiwa kusaidiwa kuandika kutokana na makosa yao angalia wameandika COVIK ONE NINE, kitu ambacho si kweli," amesema.

## Huyu ndiye Kenny Rogers


NI wiki ya majozi! Unaweza kusema hivyo baada ya dunia kushuhudia wakongwe watatu wa muziki wakiaga dunia katika muda wa wiki moja pekee.

Kati ya wasanii hao wakubwa waliofariki ni nyota wa muziki wa Country, Kenny Rogers kutoka Marekani.

Rogers amefariki dunia akiwa na Umri wa Miaka 81, akiwa Nyumbani kwake.

Alitamba katikia miaka ya 1970 na 1980, alishinda tuzo za Grammy tatu kutokana na kazi zake nzuri kama The Gambler, Luccie na Coward of the Country.

Rogers alikuwa mwandishi wa nyimbo, muigizaji, muimbaji na mtayarishaji wa muziki.



MAKALA

# Makundi hatarishi yanavyoweza kujikinga na corona kwa usahihi

**Na Mwandishi Wetu**



VIRUSI vya COVID 19 vinaendelea kusambaa katika nchi nyingi duniani. Serikali zinafanya kazi kubwa kuelimisha wananchi wao kuchukua hatua ya kujikinga na ugonjwa huo.

Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizoathirika na Corona na katika takwimu za hivi karibuni jumla ya wagonjwa 13 wamepatikana na wengine kadhaa kuwekwa katika karantini za kuchunguzwa afya zao.

Katika hatua ambazo serikali imezichukua ni kuzuia mikutano ya hadhara, kufunga shule zote na vyuo vikuu, kuzuia mikusanyiko inayohusu michezo, semina na makongamano.

Aidha, imewataka watu kujihadhari kwa kufuata masharti ya usafi kwa kunawa mikono kila wakati, kutumia dawa ya kutakasa mikono, kutumia vitambaa vya usoni kama na kuhimiza watu kuwa waangalifu kwenda maeneo yenye msongamano.

Hayo yote ni kutaka raia wake kujikinga na virusi vya corona ambavyo ni hatari kutokana na kushambulia mifumo ya hewa.

Wataalamu wanasema virusi vya corona vinaweza kumuathiri mtu yeyote, lakini watu wenye magonjwa mengine na wazee wapo hatarini zaidi kuathirika.

Watu wenye umri wa miaka zaidi ya 70 na wale wenye maradhi ya ubongo na watu walio chini ya umri wa miaka 70 wapo katika hatari zaidi ya kupata maambukizi.

Watu wameshauriwa kujilinda dhidi ya coronavirus ili kukabiliana na hatari ya maambukizi yake na kuenea kwake.

**WAGONJWA WA PUMU**

Mamlaka ya afya nchini Uingereza imewashauri watu wenye pumu kutumia tiba ya 'inhaler' mara kwa mara.

Hii itasaidia kuzuia uwezekano wa mtu kukutwa na tatizo la kupumua linalosababishwa na virusi kama vile vya corona.

Anatakiwa kuhakikisha kuwa 'inhaler' yake ipo karibu naye kila siku hata iwapo hana dalili za pumu.

Iwapo Pumu imekuja na makali na umegundua kwamba umeathirika na maambukizi ya virusi vya corona wasiliana na maofisa wa afya.

**WAZEE WATAFANYAJE?**

Ushauri unaotolewa na wataalamu wa afya ni kukaa mbali na wenye maambikizi.

Hatua hii ina maana ni hatari kwenda katika maeneo yenye msongamano wa watu.

Watu wenye umri wa miaka 70 kwenda juu pamoja na watu wenye maradhi mengine wako hatarini kuambukizwa katika maeneo kama hayo.

Watu wanaoonyesha dalili za maambukizi kama kukohoa na mafua wanatakiwa kukaa nyumbani na kujitenga.

**WAGONJWA WA KISUKARI**

Watu wenye aina ya kwanza na ya pili ya ugonjwa wa kisukari wako katika hatari kubwa ya kuathirika na corona.

Dan Howarth , Mkuu wa Kituo cha Ugonjwa wa Kisukari nchini Uingereza anasema kwamba Covid-19 inaweza kupunguza kasi ya kisukari.

Iwapo unaugua kisukari na unaona dalili kama vile kukohoa na joto jingi mwilini pamoja na kushindwa kupumua, ni vyema kwenda haraka hospitali kupima afya yako.

**WAJAWAZITO WAPO HATARINI?**

Hakuna ushahidi kwamba wanawake wajawazito na watoto walio tumboni wapo katika hatari ya kuambukizwa na virusi vya corona, lakini serikali zimewaomba kuchukua tahadhari za kiafya.

Kama watu wengine wajawazito wanapaswa kuchukua tahadhari ili kuzuia maambukizi.

Wameorodheshwa katika orodha ya watu walio katika hatari ya kupata maambukizi, kulingana na maofisa wa afya.

Iwapo mwanamke ana ujauzito wa chini ya wiki 28 na haugui ugonjwa wowote, unatakiwa kukaa mbali na mkusanyiko wa watu. Hata hivyo anaweza kuendelea kufanya kazi huku ukichukua tahadhari kwa kutumia vifaa vya kumlinda.

Iwapo ana ujauzito wa zaidi ya wiki 28 au ana matatizo kama vile figo , au ugonjwa wa mapafu anatakiwa kujitenga na watu walioambukizwa virusi vya corona.

**HATARI YA VIFO**

Utafiti wa sasa unakadiria kuwa kati ya kila watu 40 wanaweza kufa kati ya 1000 waliopata virusi vya corona.

Waziri wa afya wa Uingereza, Matt Hancock anasema serikali yake itafanya uchunguzi vizuri na kuangalia kupunguza idadi hiyo na kufikia asilimia mbili au chini ya hapo.

Watu wanaofariki wengi wao wanakuwa na matatizo mengine au umri kuwa mkubwa.

Katika kiwango cha elimu ya juu ni ngumu kubaini idadi ya watu wanaopoteza maisha kutokana na corona.

Hata hivyo ni vigumu kujua idadi sahihi ya watu wanaofariki kufuatia wengi kuwa na tabia ya kutokwenda hospitali wanapopata dalili za ugonjwa huo.

Kwa mujibu wa tafiti zilizofanywa na chuo cha Imperial, zinasema kuwa mataifa mbalimbali ambayo yameathirika vibaya na ugonjwa huo ni ngumu kuhesabu wagonjwa wote.

Lakini kuna majibu tofauti pia katika kila ushahidi, ambao unaweza kuongeza nafasi za kuonyesha picha halisi ya tatizo lililopo.

Kama utatumia takwimu za Hubei peke yake, eneo ambalo vifo vilivyosababishwa na corona vilikuwa juu zaidi ya maeneo mengine ya China, basi makadirio ya vifo yangekuwa mabaya zaidi.

**Kwa msaada wa mitandao**

# Uchaguzi 2020 vyama visisahau wanawake

Na Sabato Kasika

OKTOBA mwaka huu, taifa linatarajia kufanya uchaguzi mkuu wa kumpata rais, wabunge na madiwani. Ni wakati wa vyama vya siasa kuachana na mazoea ya kujisahau na kuwaweka wanawake pembeni badala yake vitoe nafasi za kutosha kwa wanawake kuwania uongozi.

Wadau wa usawa wa kijinsia wanaona kuwa kuna umuhimu kwa wanawake kugombea nafasi za kisiasa katika ngazi mbalimbali kuanzia serikali za mitaa, udiwani, ubunge na urais.

Wanawapa moyo wanawake na wagombea vijana wa kike kuwa linapokuja suala la wanawake katika uongozi ni lazima kuwa mstari wa mbele kulipigia chapuo.

"Wito wangu kwa vyama vya siasa nchini ni kupanua wigo kwa wanawake kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya vyama hivyo kuanzia kata, majimbo na urais," anasema Lilian Liundi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) anasema, Afrika, ikiwamo Tanzania, wanawake ni zaidi ya asilimia 50, hivyo hawawezi kuachwa nyuma katika vyombo vya maamuzi.

Aidha, anawataka vijana wa kike kutobaki nyuma na badala yake wajiunge na vyama, kwa vile siyo rahisi kupata uongozi bila kuwa mwanachama wa chama cha siasa.

Liundi anasema, TGNP ina mikakati mingi ya kutaka kuhakikisha wanawake wanapata nafasi za kutosha za kisiasa.

Anasema, mtandao huo una Ilani ya Uchaguzi ya Wanawake ambayo imesambazwa kwa wadau mbalimbali wa uchaguzi vikiwamo vyama vya siasa ili kuangalia yaliyomo na kuyafanyia kazi.




Wadau wa kutetea haki za wanawake wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kumaliza mkutano.

### KUACHA UBURUDISHAJI

"Ilani hii inatuhamasisha sisi wanawake, wapigakura kutoendelea kutumiwa kama wapigadebe na waburudishaji kwenye sherehe au kampeni za uchaguzi," anaonya Liundi.

Anasema, umefika wakati wanawake wakiwamo vijana wa kike kuhamasika na kushikamana ili kupambana na mifumo kandamizi hususani mfumo dume, ambao huathiri upatikanaji wa haki za wanawake na hatimaye kudumaza uchumi na maendeleo ya jamii yote ya wake kwa waume.

Anasema, ni wakati wa kuhakikisha wanawake wanapata nafasi za uongozi kwa vile wana uwezo kama walivyo wanaume na kwamba ilani hiyo inalenga vyama vya siasa, tangu wanachama, uongozi na mashabiki wa vyama hivyo.

"Ikumbukwe kwamba hapa nchini vyama vya siasa ni njia pekee ya kuingia kwenye kinyang'anyiro cha uchaguzi, vyama hivyo ni walinzi wa lango kuu la kuingia kwenye siasa za uchaguzi, na ndiyo maana tunavitaka vipanue wigo ili kuwapa nafasi wanawake kuwania uongozi," anasema Liundi.

### WAJIBU WA VYAMA

Liundi anasema vyama vya siasa ndivyo huamua nani aingie, au aachwe, nani awezeshwe kushinda na pia ni nani aachwe akiogelea mwenyewe kwenye uwanja wa ushindani usiyo haki na huru kwa wanawake walio wengi.

Anaeleza kuwa ilani hiyo pia inalenga vyombo vya habari kutokana na uwezo wa vyombo hivyo kwa vile vinagusa mtazamo wa jamii kuhusu nafasi ya wanawake katika uongozi na maendeleo ya taifa kwa ujumla.

"Kwa hiyo nitoe wito kwenu vijana wa kike msibaki nyuma jiungeni na vyama vya siasa kwa ajili ya kutafuta uongozi ili kupata uwiano katika uongozi wa nchi hii bila kujali jinsia," anasema.

### UONGOZI

Mkurugenzi mtendaji wa TGNP anasema, ushiriki wa wanawake katika nafasi za maamuzi hasa wa kisiasa, bado ni mdogo, hali ambayo inakinzana na azma ya kujenga jamii isiyokuwa na ubaguzi kama ilivyobainishwa kwenye dira ya Taifa 2025, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977, pamoja na sheria mbalimbali za nchi.

Hata hivyo, anasema kwenye awamu ya tano, katika ngazi zote za uongozi, wanawake ni asilimia ndogo, lakini chaguzi wa mwaka 2015 ulivunja rekodi kwa kupata Makamu wa Rais wa kwanza mwanamke tangu kupata uhuru.

"Mawaziri ni asilimia 17, makatibu wakuu ni asilimia 11, wakuu wa mikoa asilimia 23, kulinganisha na asilimia 28.5 kipindi cha 2010/2015, wakuu wa wilaya ni asilimia 28, toka asilimia 35.3 katika kipindi cha 2010/2015," anasema.

Anasema, ushiriki wa wanawake katika siasa na uchaguzi ngazi ya ubunge, wanawake wanaoteuliwa na vyama vya siasa kuwania nafasi ya ubunge wa kuwakilisha jimbo ni ndogo, na hatimaye wanaoshinda ni kidogo zaidi.

"Ni wanawake wachache sana huteuliwa na vyama vyao kuwania nafasi za uchaguzi. Kwa mfano, katika uchaguzi wa mwaka 2015, vyama viliteua wagombea wanawake kama ifuatavyo:- CCM asilimia tisa, Chadema asilimia sita, CUF asilimia 11 na ACT Wazalendo asilimia 15," anasema.

Anasema, pamoja na kwamba viti maalum vimewezesha kuongezeka kwa uwakilishi na sauti za wanawake katika muhimili mkuu wa utawala, utekelezwaji wake umekuwa na changamoto.

"Wawakilishi wanaopitia viti maalum hubaguliwa kushika baadhi ya nyadhifa kama waziri mkuu, hubaguliwa katika kupewa fedha za majimbo, na kwenye baadhi ya vyama vya siasa hakuna uwazi kwenye uteuzi wao," anasema.

### VYAMA VINGI

Liundi anakumbusha kuwa azma ya kuanzishwa kwa siasa ya vyama vingi ni kujenga demokrasia shirikishi inayoongozwa na misingi ya usawa, utawala bora na kuheshimu haki za binadamu.

Hata hivyo kuanzishwa kwa vyama vingi hakujaleta mabadiliko makubwa kwenye usawa wa jinsia, heshima ya haki za wanawake na makundi yaliyoko pembezoni, wala ushiriki wa wanawake na makundi ya pembezoni katika uongozi wa vyama.

"Mfano mmojawapo ni kwamba, tangu kuanzishwa kwa vyama vingi, nafasi ya wenyeviti wa vyama imehodhiwa na wanaume, isipokuwa chama kimoja kilichomchagua mwanamke kama mwenyekiti ambaye hakuwa msemaji wa mwisho wa Chama husika," anasema.

Liundi anasema, kuna vyama vitatu na kwamba ni asilimia 16 tu yenye wanawake walioshika wadhifa wa ukatibu mkuu wa vyama vyao kati ya vyama 19.

Kwamba kati ya manaibu wasaidizi 38 wa vyama vya siasa, kuna wanawake 4 tu sawa na asilimia 14 ya manaibu katibu wakuu wa vyama, wanawake ni wachache kwenye nyadhifa za ukurugenzi na shughuli nyingine zinazohitaji uongozi.

"Lakini cha kushangaza ni kwamba vyama vyote vinategemea sana nguvukazi ya wanawake katika kuhamasisha wanachama, katika kutafuta rasilimali fedha na katika kampeni za vyama wakati



Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi, wakati akihimiza vyama vya siasa kupanua wigo kwa ajili ya nafasi za uongozi kwa wanawake. Kulia ni Ofisa Progamu Mwandamizi wa mtandao huo na wadau wengine wa kutetea haki za wanawake. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

MAKALA

# Licha ya kujifariji na visingizio maziwa, nyama ni vya lazima

**Na Gaudensia Mngumi**

MAZIWA ni chakula ambacho wengi hukikosa kutokana na kuhofia kuwa hayana viwango au huenda yamechanganywa na maji, mengine ni machafu yana taka hasa mbolea kwa vile wapo wanaokamua wanyama bila kusafisha kiwele.

Hofu nyingine ni kutochemshwa kwani baadhi ya wauzaji hawajali afya za walaji na bila kujali kuwa maziwa huambukiza kifua kikuu (TB) huuzia watu bila hofu maziwa ambayo hayajachemshwa.

Yote haya huwafanya wakazi wengi wa mijini kuogopa kunywa maziwa halisi ya ng'ombe huku wakikimbia ya paketi kwa kisingizio cha bei na kuifanya Tanzania kuwa taifa lisilokunywa maziwa licha ya kuwa na ng'ombe takribani milioni 30.

Mwishoni mwa mwaka jana kulikuwa na taarifa za mashine au ATM za kutolea maziwa zilizoanza kufanyakazi mkoani Kilimanjaro.

Kinamama wawekezaji mkoani humo walianza kuuza maziwa hayo katika mtaa wa Chagga mjini Moshi huku kukiwa na ATM nyingine wilayani Hai na jijini Arusha.

Ni maziwa halisi yaliyoandaliwa kitaalamu ambayo pengine ni vyema yangefikishwa kwenye miji mingi na majiji yote kwa kuwa unywaji maziwa si jambo linalotiliwa maanani na wakazi wengi mijini.

Maziwa hayatiliwi maanani kwa vile upatikanaji wa bidhaa hiyo hasa maeneo ya mijini ni mgumu kwani wauzaji hawazingatii viwango wala ubora.

Kwa mfano jijini Dar es Salaam, unaweza kununua maziwa kwenye mgahawa lakini yamechanganywa na maji, ukauziwa kwa Sh. 1,000 kwa kikombe lakini ukaambulia kunywa maji meupe yenye matone machache ya maziwa.


Kwa vijijini hasa kwenye wafugaji maziwa yapo lakini ni kwa nadra watu hunywa maziwa mabichi kama kinywaji na kuyafurahia.

Wengi hupendelea ama kuweka kwenye chai au kutumia mtindi zaidi. Kuna sehemu nyingine maziwa huchukuliwa kama chakula cha watoto na kinamama.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, inahimiza watu kutumia chakula hiki na kwamba maziwa si kwa ajili ya watoto bali kila mmoja anapaswa kunywa lita 200 kwa mwaka.

Mwaka wenye siku 365 ni kama zote mtu anatakiwa kupata angalau nusu lita ya maziwa kila siku kwa afya.

Pamoja na maziwa Shirika la Kilimo la Umoja wa Mataifa ( FAO) linaelekeza kuwa pamoja na maziwa ni vyema pia kula nyama kilo 50 na mayai 300 kwa mtu kwa mwaka.



Maziwa ni muhimu kwa ukuaji na afya ya mwili kwa watoto na wakubwa kwa vile yana virutubisho muhimu ikiwamo madini ya kalishamu yanayoimarisha mifupa. **PICHA MTANDAO.**

Kwa maelezo hayo ya Wizara na WHO kuhusu maziwa, nyama na mayai pengine kitu ambacho Watanzania wengi hasa wa mijini wanaweza kujivunia ni ulaji wa mayai.

Hii ni kwa sababu chakula kikuu ni 'chips na mayai au zege' ambalo ni mchanganyiko wa wastani wa mayai mawili kwa kila linapoandaliwa.

Licha ya kwamba watu wengependa kutumia maziwa kwa mijini chakula hicho pamoja na kuuzwa ghali kinachakachuliwa , kwa vile hujazwa wakati maziwa ya mtindi huchanganywa na unga wa ngano.

Pamoja na ukweli kuwa maziwa yanapatikana mijini hasa ya mifugo kuna yanayojazwa maji, mengine huchanganywa na ya unga, lakini mengine hukamuliwa kwa uchafu na kama ni mtindi hayachemshwi kiasi cha kumkera mteja anayetumia kwani anaweza kuugua tumbo la kuhara.

Wakazi wa mijini wana cha kusingizia lakini wale wanaoishi vijijini kwanini wasitumie maziwa? Ni changamoto inayowahusu wote kwa kuwa kila mmoja anawajibika kujibidiisha kupata protini hizi.

Kwa mujibu wa mtandao wa Wikipedia kunywa maziwa wakati wa mvua kama hizi zinazoendelea kunyesha msimu huu wa maasika majani yanapochipuka ni jambo bora kiafya kwa pamoja na virutubisho yana dawa.

Inaelezwa kuwa maziwa haya yana virutubisho vya kila aina na pia yana dawa za aina mbalimbali kutokana na mifugo kula aina nyingi za majani ikiwamo miti na nyasi dawa.

Watu wanashauriwa kunywa maziwa mabichi (freshi) msimu huo ili kusisimia mifumo mbalimbali ya mwili inayotibiwa kwa lishe ambayo ni tiba mbadala.

Kwa hiyo ili Watanzania waanze kujiweka kwenye viwango vinavyopendekezwa na FAO ni budi kuanza kunywa na kula kwa kuhesabu kiasi unachotumia ili uende kwa misingi na maelekezo ya wataalamu.

**NYAMA MBADALA**

Ulaji wa nyama kwa Watanzania wengi unaweza kuwa mgumu kwa vile wengi wanaona kitoweo hiki ni ghali na ni chakula kinachohusishwa na familia zenye uwezo kifedha, jambo ambalo ni kweli kwa vile kilo moja ya kitoweo mijini ni karibu 7,000 wakati vijijini nako huuzwa takribani Sh 6,000.

Ni wazi kuwa siyo lazima kula nyama ya ng'ombe, mbuzi, kondoo au nguruwe lakini ni muhimu kula nyama kwa hiyo kuna haja ya kufuga wanyama wadogo kama kware, bata, kuku wa kienyeji, sungura, mbuzi, kondoo ambao kila mmoja anaweza kuwafuga akiamua.

Miradi hiyo inayotekelezwa kupitia program ya kuendeleza mifugo midogo inayofanywa kwa kushirikiana na serikali za mitaa.

Kwa hiyo inavyoelekea siyo kazi ngumu kupata kilo 50 za nyama kwa mwaka kwa vile watu wanaweza kufuga na kula wanyama wadogo kama sungura, simbilisi, mbuzi na kondoo hata wanaoishi mijini.

Lakini pia, ndege wakiwamo kware, kanga, bata na njiwa nao wanaweza kuimarisha mlo kwa kuongeza kitoweo na kuwafanya Watanzania kuondokana na tatizo la lishe duni , kudumaa na utapia mlo.

Wanyama kama mbuzi wanatoa maziwa ambayo ni chakula bora kwa watoto wachanga, wagonjwa na wazee pamoja na wanafamilia, mbuzi nao wanafugika mijini.

**KULA KIAFYA**

Hata hivyo siyo lishe bora kunywa lita mbili za maziwa kila siku au kula mayai matano na chips au kutafuna ugali na pande la nyama la kuchoma yenye uzito wa nusu kilo kila siku.

Ulaji uzingatie afya kwa kuwa kula bila mpangilio kunaleta unene kupindukia na magonjwa hasa ya mifumo ya damu, moyo na misuli.



Kutoka kushoto ni Ursula Komuhangi, Credonia Mwerinde, Joseph Kibwetere na Dominic Kataribabo

# Miaka 20 mauaji Kibwetere Waganda walia na wachungaji

**Na Mwandishi Wetu**

MACHI 17, 2000, Uganda ilitikiswa na tukio la kutisha baada ya mamia ya wanachama wa dhehebu la Amri Kumi za Mungu, kuteketea kwa moto ndani ya kanisa.

Waumini hao wakiongozwa na kiongozi wao Joseph Kibwetere, walijifungiandani kanisa moja, na kisha kujitekekeza kwa moto nyakati za mchana.

Takwimu zilizotolewa na polisi baadae, zinasema zaidi ya watu 700 walipoteza maisha, lakini huenda idadi ilikuwa kubwa.

Makao makuu ya kanisa hilo yako eneo la Kanungu, kusini-magharibi mwa Uganda. Kabla ya kujiteketeza kwa moto, waumini hao waliambiwa wauze mali zao zote kwa sababu mwisho wa dunia ulikuwa umefika.

Miaka 20 sasa imepita tangu kutoke kwa tukio hilo, lakini bado limekuwa kidonda kikubwa kwa Judith Ariho, ambaye bado anakumbuka machungu kutokana na tukio hilo.

Hata hivyo, katika kipindi chote hakuna mtu aliyeshtakiwa kwa kuhusishwa na mauaji hayo, na haijafahamika kama kuna viongozi wa kanisa hilo ambao wapo hai au nao wamekufa.

Anna Kabeireho, ambaye bado anaishi eneo la milimani, ameiambia BBC kuwa hajasahau tukio hilo, harufu ya moshi inaendelea kuganda kwenye pua yake.

"Siku ile ya Ijumaa kila kitu kilikuwa kimefunikwa kwa moshi na harufu ya nyama mbichi ilikuwa imetanda. Yaani harufu kama ilikuwa inaingia kwenye mapafu," anasema.

Anaendelea kukumbuka "Kila mtu alikuwa anakimbilia katika bonde la maji. Moto ulikuwa unaendelea.Miili mingi ilikuwa imeungua na hata hawakujulikana walikuwa ni kina nani,"

Anakumbuka watu walikuwa wamefunika pua kwa majani ya migomba ilikuzuia harufu. Kwa miezi kadhaa hawakuweza kula nyama.

Kanungu ni sehemu yenye ardhi ambayo ina rutuba , lakini amani iliondoka baada ya kuzuka kwa moto huo.

Kanisa hilo liliundwa mwaka 1980 na watu wawili ambao ni Credonia Mwerinde, mhudumu wa zamani kilabu cha pombe na Joseph Kibwetere, ambaye alikuwa mfanyakazi wa zamani wa serikali.

Kanisa hilo lenye mlengo wa Kikaresmatiki halikuwa na uhusiano mzuri na kanisa katoliki. Wahudumu wake walikuwa mapadri na watawa ambao walitengwa na kanisa hilo wakiwe mo Ursula Komuhangi na Dominic Kataribabo.

Waumini walikuwa kimya, walipokuwa wanatumia njia ya kuwasiliana.

Ariho, kwa sasa ana miaka 41, alijiunga na kundi hilo pamoja na familia yake akiwa na miaka 10.

Mama yake ambaye alikuwa mjane alikuwa anahangaika kuwalewa watoto wake watatu.

Mmoja alikuwa anasumbuliwa na matatizo ya kichwa kila mara.

Aliingia katika kundi la Kibwetere kwa ajili ya maombi.

Jumuiya hiyo ilichukua familia yote na kuisaidia katika mahitaji yao kuanzia kwenye ada za shule mpaka chakula. "Tulifanya kila kitu ilii kujizuia kutenda dhambi. Wakati mwingine ukifanya dhambi unapaswa kusali rozari mara 1,000.

Ilikuwa kama adhabu na ulikuwa unaomba rafiki zako au familia kukusaidia kusali rozari," anasema

Anasema anakumbuka kuna familia ambayo ilipoteza mama na watoto 11 Haijafahamika nini kilikuwa nyuma ya mauaji hayo, kwani watu wengi wanamuelezea Kibwetere kuwa alikuwa mtu mwenye mafanikio na muumini wa kawaida wa kanisa katoliki.

Kilichowakumba waumini hao na hivi sasa kubaki kama mashahidi wa imani potofu, inazidisha hofu na kuendelea kuchipuka kwa makundi ya kidini ambayo mafundisho yao yanaleta shaka.

Kuna baadhi ya viongozi wa nyumba za ibada wanatumia nafasi zao za kuaminiwa na waumini wao kutoa mafundisho ambayo kimsingi yanaweza kuleta maafa kwa jamii kama serikali haitachukua hatua za haraka.

Keneth Mchambo, mkazi wa Tabata, anasema mauaji ya kanisa la Kibwetere, hayakuja kama kwa ghafla kwani kulikuwepo na ulishaji wa imani mbaya kwa muda mwingi na hatimaye watu wakaamini.

"Kuna baadhi ya nyumba za ibada zinatumika kutoa mafundisho yanayokwenda kinyume na misingi ya imani za Mungu na utu wa mtu, haiwezekani watu wakalishwa nyasi au wakaambiwa vitu fulani vinaweza kuwaponya huku ikijulikana si kweli," anasema Mchambo.

Joseph Mlamapori, kwa upande wake anasema kumbukizi hizo kuwepo na tafakari ya kina kama kumeleta fundisho chanya kwa jamii yetu au la.

"Tuangalie namna baadhi ya makanisa yetu yanavyofanya, je ni kweli wanakwenda na mafundisho ya Mungu? Jibu rahisi ni hapana, kuna mashaka mengi kutokana na viongozi kuwa na imani zinazoonekana kuwayumbisha waumini wao," anasema.

Hivi karibuni Rais Dk. John Magufuli, alisisitiza hakuna umuhimu wa kuzifunga nyumba za ibada, badala yake kuwepo na udhibiti kwa mafundisho yanayotolewa kinyume na misingi ya kiungu.

Rai Magufuli aliwataka wananchi kuwa na tahadhari pale inapotokea viashiria vya hatari katika nyumba hizo.



## HABARI KIMATAIFA

# Waziri mkuu Uingereza akutwa na Corona

**LONDON,** Uingereza

WAZIRI Mkuu wa Uingereza, Borris Johnso, amekutwa na virusi vya corona baada ya kufanyiwa vipimo.

Katika taarifa iliyotolewa na ofisi yake iliyopo mtaa wa Downing, imesema kiongozi huyo ana dalili ndogo za ugonjwa wa corona.

"Nimekuwa na dalili ndogo za corona, ambazo ni viwango vya juu vya joto la mwili na kikohozi ambacho hakikomi ", Johnson amesema katika video aliyoituma kwenye ukurasa wake wa Twitter.

**Ninaweza kuendelea, nashukuru teknolojia kwamba ninaweza kuwasiliana na viongozi wakuu na kuongoza taifa dhidi ya virusi.**

Waziri Mkuu huyo wa Uingereza alisema ataendelea kuliongoza taifa kutoka nyumbani kwake baada ya kupatikana na ugonjwa wa Covid-19.

Johnson atajitenga katika makao yake ya kikazi baada ya kupimwa na kupatikana na virusi hivyo na kuanza kupatiwa huduma za afya katika ofisi yake maarufu kama Namba 10.

Licha ya kupata maambukizi, Johnson ataendelea kuwa mkuu wa shughuli za kukabiliana na corona nchini humo.

"Ninafanyakazi kutoka nyumbani na nimejitenga. Hilo ndio jambo sahihi la kufanya". Alisema na kisha aliendelea "Ninaweza kuendelea, nashukuru teknolojia kwamba ninaweza kuwasiliana na viongozi wakuu na kuongoza taifa dhidi ya virusi.",

"Kwa hiyo nashukuru sana kwa kila mtu anayefanya kile ninachokifanya kutoka nyumbani ili kuzuwia maambukizi ya virusi kutoka nyumba moja hadi nyingine", aliongeza.

Johnson alipima afya yake baada ya kushauriwa na mshauri Mkuu wa tiba wa nchi hiyo, Profesa Chris Whitty, imesema ofisi yake. **BBC**



Polisi wakiwaondosha kwa nguvu wanawake wawili wauza matunda katikati ya jiji, baada ya kukiuka amri ya kukaa nyumbani kwa siku 32 iliyotolewa na Rais Yoweri Museven, katika kukabiliana na COVID-19. **PICHA: AFP**

# Afrika Kusini yatangaza vifo viwili

**CAPE TOWN,** Afrika Kusini

AFRIKA Kusini imetangaza vifo vya wagonjwa wawili waliougua ugonjwa wa corona.

Taifa hilo limeanza kutelekeza amri ya kutotoka nje, idadi wa watu walioambukizwa virusi vya corona wakifikia 1,000.

Jeshi la nchi hiyo limeanza kufanya kazi ya kusimamia amri hiyo ikiwa ni hatua ya kupambana kuenea kwa maambukizi ya virusi hivyo.

Kabla ya kuanza kutekelezwa kwa agizo hilo, foleni ndefu ya watu ilionekana kwenye maduka makubwa wakifanya manunuzi muhimu ili kujiwekea akiba wakati wakiwa nyumbani.

Juzi Rais Cyril Ramaphosa, alitembelea kambi ya jeshi kabla askari hao kuruhusiwa kuingia barabarani,

"Ninawatuma kwenda kuwalinda watu wetu na virusi vya Corona,"Alisema hayo akiwa amevalia sare za jeshi.

"Ni wakati mbaya kwa demokrasia yetu, lakini pia kwa historia ya taifa letu kwamba tutaifunga nchi yetu kwa siku 21 ili kupambana na adui asiyeonekana, virusi vya corona" aliongeza.

Alisema maduka ya vyakula hayatafungwa ingawa maduka yanayouza vilevi yamepigwa marufuku kufunguliwa kwa siku 21. **BBC**

## G20 yaahidi trioni 5 kuokoa ajira

**BERLIN,** Ujerumani

Nchi za G 20 kuweka zaidi ya dola trilioni 5 katika uchumi wa dunia kuzuia kuporomoka kwake

VIONGOZI wa mataifa yaliyoendelea kiuchumi ya G20, wameahidi kuweka zaidi ya dola trilioni tano kuzuia ukosefu wa ajira kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Katika mkutano wao huo, wameahidi kufanya kila wanaloweza kuhakikisha wanakabiliana na kuenea kwa virusi hivyo.

Kupitia mkutano wa kilele uliofanyika kwa njia ya video, viongozi hao wameonyesha mshikamano zaidi tangu muungano huo wa G20 ulipoanzishwa.

Rais wa China, Xi Jinping, ni miongoni mwa viongozi walioshiriki mkutano huo. **DW**

## Marekani yaongoza wagonjwa wa corona

**WASHINGTON,** Marekani

MAREKANI imethibishwa kuwa na wagonjwa 85,500, ambao ni wengi kuliko nchi nyingine yeyote duniani.

Kwa mujibu wa tawimu zilizokusanywa na chuo kikuu cha Johns Hopkins, nchi hiyo imeipiku China ambayo ina wagonjwa 81,782 na Italia 80,589 ya waliothirika na virusi vya Covid 19.

Kati ya idadi hiyo, wagonjwa 1,300 wamekufa kutokana na ugonjwa huo na kuifanya Marekani kuwa na idadi ndogo ya vifo ukilinganisha na China 3,291, huku Italia ikiripoti vifo 8,215.

Idadi hiyo ya maambukizi inapingana na kauli ya Rais Donald Trump, ambaye alisema anategemea hali itakuwa shwari muda si mrefu.

Makamu wa Rais, Mike Pence, alisema vipimo vya utambuzi wa virusi vya corona katika majimbo yote 50 na zaidi ya watu 552,000, wamepimwa.

Trump amekosolewa kwa hatua yake ya kutaka vizuizi vya kukaa nyumbani viondolewe April 12 wakati wa sikukuu ya Pasaka. **BBC**

## China yataka maridhiano na Marekani

**BEIJING,** China

RAIS wa China, Xi Jinping, ametaka kuwa na mazungumzo na Marekani yenye lengo la kuboresha uhusiano.

Wizara ya mambo ya nje ya China, imesema Rais Xi Jinping, amezungumza kwa simu na kiongozi wa Marekani, Donald Trump, jana na anataraji nchi hizo zitaboresha ushirikiano wao.

Xi alisema ushirikiano kati ya nchi hizo ndiyo njia sahihi ya kwamba China iko tayari kuisaidia Marekani katika kukabiliana na virusi vya corona. Mazungumzo hayo ya simu kati ya viongozi hao wawili yamekuja wakati kuna vita vya maneno vinavyoendelea kuhusiana mambo tofauti ya kiuchumi na virusi vya corona vilivyoibuka mwishoni mwa mwaka jana huko China.

Trump na maofisa wengine wa ngazi ya juu wameituhumu China kwa kutokuwa na uwazi kuhusu virusi hivyo ambavyo vimewauwa zaidi ya watu 24,000 duniani kote. **DW**



# HADITHI

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote. Afanye chochote kile ili awenavyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele. Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo.

Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

# MAUAJI HARUSINI-6

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**




**Na Adam Fungamwango**

Ilikuwa ni hatua 50 tu ambazo bwana na bibi harusi walikuwa wamezipiga kuelekea kwenye hema kubwa la kisasa lenye nakshi, lililokuwa nje ya jumba la fahari.

Geti lilikuwa wazi ili kuwawezesha umati wa wahudhuriaji kuingia ndani ya uwanja mkubwa, lakini baadhi ya magari, hasa mabasi mkubwa yakiwa yamebaki nje ya geti, lakini baadhi ya magari madogo yakiwa yameruhusiwa.

Ilikuwa ni tafrija ya nyumbani kwa siku hiyo, huku kesho yake kukiwa na sherehe kubwa kwenye hoteli kubwa ya kifahari katikati ya jiji la Dar es Salaam.

Ghafla sauti kali isiyotarajiwa sehemu kama hiyo ikasikika. Kabla yoyote yule hajajua ni ulikuwa ni mlio wa kitu gani, mlio mwingine unaofanana na ule ukarindima. Hakuna aliyejua nini kimetokea.

Ilikuwa imetimia saa 11:00 jioni. Ni mlio uliosababisha baadhi ya watu kusambaratika huku na huko, kila mmoja kuokoa uhai wake.

Haukuwa mlio wa kawaida. Lakini walichotambua ni kwamba haukuwa mlio wa heri, bali ni wa shari, unaoashiria hatari. Kila mmoja aliyekuwa kwenye sherehe hiyo hakujua anakimbilia wapi au anaelekea wapi. Ilichukua dakika nyingi sana kutambua milio ile miwili ilikuwa ni ya bastola.

**Ni kitendo bila kuchelewa, kwani wakati watu hajajui nini kinaendelea, aliachia nyingine kwenye paji la uso la bi harusi. Yeye alianguka kama mzigo, amlalia mumewe.**

Baada ya dakika kadhaa eneo ambalo watu walikusanyika kwa ajili ya sherehe za harusi lilikuwa wazi. Kila mtu alikimbia kwa nguvu zake zote alizojaaliwa.

Ni watu wawili tu ambao walishindwa kukimbia au kujificha. Ni bwana na bi harusi. Walikuwa wamelala chini.

Haikujulikana mara moja kama walikuwa chini kwa sababu ya kukanyagwa au vipi. Lakini milio miwili la bastola ndiyo ilitia watu wengi wasiwasi.

Yoyote aliyedhania kuwa walikuwa wamekanyagwa na kundi la watu waliokuwa wakikimbia na kujipapatua kwa kuogopa kifo walikosea.

Haikuhitaji hata cheti cha udaktari kujua kuwa waliolala hapo tayari walikuwa ni marehemu. Bwana harusi alilala chali chini ya sakafu, huku mkewe aliyetoka kumuoa masa machache yaliyopita akilala juu ya mwili wake.

Ilionekana kabisa kuwa bwana harusi alikuwa ameanguka chini na baadaye bi harusi akafuata.

Chini kulikuwa na kijito cha damu ambacho yoyote aliyekiona, hawezi kukubali kuwa watu hao walikuwa hai.

************************************

Alikuwa ameteremka kwenye bodaboda akiwa kama mmoja wa waalikwa kwenye harusi hiyo. Hakupanda kwenye gari ili kukwepa kufuatiliwa zaidi na watu. Mara nyingi kwenye sherehe za harusi, au mkusanyiko wa watu kama huo kuna baadhi ya watu kazi yao ni kuangalia uzuri wa magari, pamoja na watu walioteremka, kuliko kuangalia harusi yenyewe.

Wakati huo maharusi walikuwa wameshateremka kwenye gari la kifahari, wakiwa na nguo za kifahari, wakitembea kwa madaha, kama mfalme na malkia hivi.

Pembeni mwa bwana harusi kulikuwa na mpambe wake na bu harusi pia alikuwa na mpambe wake. Nyuma ya bi harusi kulikuwa na watoto wanne waliozidi miaka mitano, wawili na kiume na wawili wa kike waliokuwa wameshikilia sehemu ya shela la bi harusi ambalo lingekuwa linaburuzika chini kama si wao kulishikilia kwa nyuma.

Karibu yao kulikuwa na baadhi ya akinamama ambao walikuwa wakiimba nyimbo mbalimbali za kuwasifu na kuwapongeza bwana na bi harusi kwa uamuzi wao wa kufunga ndoa.

Tamim Hussein alitabasamu. Halikuwa tabasamu halisi. Alijua dakika kadhaa baadaye hali hii yote ya furaha na shamrashamra itabadilika na kuwa msiba mkubwa. Msiba ambao utawaacha watu wengi wa maswali ambayo hayatakuwa na majibu.

Alijua ataifanya kazi hiyo kukamilifu. Atawapiga risasi na kuwaua wale tu ambao wanatakiwa wafe na si vinginevyo. Alikuwa na uhakika na kazi yake. Hakuwahi kukosea kwenye kazi yake hiyo.

Aligeuka nyuma ili kumtazama mtu aliyekuwa anataka kumuona. Ni kweli. Alimuona Michael akiwa anamtazama kwa makini.

Walitazamana kwa namna ambayo hakuna mtu ambaye alijua kuwa wana mawasiliano. Michael yeye alikaa tayari kumlinda Tamim kama lolote lile litatokea kwa kumwamisha kazi yake ya kuua. Lakini pia alikuwa tayari kuumaliza yoyote yule atakayeonekana kutaka kumuua Tamim. Hii ilifanya ili Tamim atekeleze kazi yake vizuri bila bugudha.

Kilichokuwa sasa kinasubiriwa ni simu tu kutoka kwa Kidaga ili amalize mchezo. Kabla hajamaliza kufikiria, simu akamtetemesha kwenye suruali. Hakuna ameweka mlio. Aliitoa na kuitazama. Ilikuwa ni ya Kidaga. Aliiweka sikioni.

"Tayari, muda umefika." Ilikuwa ni amri. Wakati huo maharusi walikuwa wamebakisha mita chache kufika kwenye eneo ambalo limetengenezwa maturubai ya kisasa kabisa kwa ajili ya sherehe hizo.

Aliminya kitufe cha simu, akaihamisha mkono wa kushoto. Mkono wa kulia, ulirudi kweny mfuko wa nyuma na kuigusaa bastola. Lakini hakuitoa. Aliona kuna kitu hakiko sawa. Akaiingiza simu mfukoni kwa mkono wa kushoto, lakini kwenye mkono huo huo, akatoa leso ya kufutia jasho.

Leso ile na mkono wa kushoto ukahama kuelekea upande wa kulia. Akatoa bastola kwa mkono wa kulia na haraka kama umeme, akagusanisha mikono yote, hivyo kastola yake ndogo ikawa imefumbatwa na leso. Haikuonekana na mtu yoyote.

Aliinua mkono wa kulia juu ambao ulionekana kuwa alikuwa ameshika leso kwa ajili ya kujifutia jasho kutokana na joto.

Alisogeza leso kidogo mbele na kuivuta kwa nyuma ili kipatikana na uwazi mbele na kupiga risasi. Alianza kumlenga bwana harusi kwenye paji la uso kwa sababu alikuwa mbele yao. Aliachia risasi moja tu ambayo haikukosea, badala yake ikaenda pale pale ilipokusudiwa. Bwana harusi aliyumba kama mlevi, kabla ya kuanguka chini taratibu.

Ni kitendo bila kuchelewa, kwani wakati watu hajajui nini kinaendelea, aliachia nyingine kwenye paji la uso la bi harusi. Yeye alianguka kama mzigo, amlalia mumewe.

Hakutaka kujisumbua kama ameshaua la. Kutokana na uzoefu wake risasi ya paji la uso alizokuwa akizipiga siku zote ziliwaua majambazi hatari na wakorofi, wenye roho mbaya zaidi ya shetani, achilia mbali bwana na bi harusi ambao hawajawahi kuua hata kuku.

Upesi yeye na Michael Sabuni walikwenda kwenye gari alilokuwa akiendesha Tofiki Seif , pembeni yake kukiwa na Kidaga na kuondoka kwa kasi.

"Bosi, tumemaliza kazi uliyotutuma, kwa sasa tunakuja kwako ili tumalizіane mzigo uliobaki." Kidaga akimtaarifu Abeshi."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**ELIMU/ MASOMO**

**REGISTRATION OPPORTUNITIES**

**KELAND NURSERY AND PRIMARY SCHOOL** located at salasala announces registration opportunities for Nursery and Primary School students. Call: 0713 327613.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA CHETI



ALDEGUNDA CLEMENCE anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.205/009 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia KIBOSHO GIRLS SEKONDARI mwaka 1990.

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: STK/RB/8694/2020.**

115683202

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**RAPHAEL JOSEPH SILAYO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 4449 DMY Chassis namba BL5046382. Engine namba. EJ20C543989.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/266550/2020.**

115683602

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA TARIME**
**MAOMBI MAKUBWA NA. 13/2020 NA MAOMBI MADOGO NA. 43/2020**

HAMISI JUMA KIRERI……………………MLETA MAOMBI

DHIDI YA

1. RASHIDI HAMISI KIRERI
2. HABIBU HAMISI KIRERI
3. ISMAILI HAMISI KIRERI
4. MAGIRI HAMISI KIRERI
5. SHANIFA HAMISI KIRERI
6. MARIAM HAMISI KIRERI……………… .WAJIBU MAOMBI

Wadaiwa ISMAILI HAMISI KIRERI, MAGIRI HAMISI KIRERI, SHANIFA HAMISI KIRERI NA MARIAM HAMISI KIRERI popote mlipo. Fahamuni kwamba mleta maombi HAMISI JUMA KIRERI ameleta maombi makubwa Na. 13/2020 na maombi madogo Na. 43/2020 dhidi yenu. Hivyo basi kama mnakusudia kupinga maombi hayo mnatakiwa mlete majibu yenu na muwepo barazani nyinyi binafsi, wakili wenu au mwakilishi anayekubalika kisheria tarehe 1/04/2020 siku ambayo mashauri hayo yamepangwa kutajwa. Endapo hamtetekeleza haya shauri litaendelea upande mmoja dhidi yenu na maamuzi kutolewa.

Imetolewa na kutiwa saini na mhuri wa Baraza hii leo tarehe 10/03/2020.

NGUKULIKE. N.O
MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) TARIME

115683402

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD, RAISSA COMPANY LTD** tutauza kwa mnada wa hadhara gari aina ya Toyota Cresta –T 572 DCJ mali ya mdaiwa sugu, Ndugu Nazael Eliaza Mngulwi, mnada huo utafanyika tarehe 03/4/2020 Lengo ni kufidia/ kupunguza deni la mkopo anaodaiwa. Mnada utafanyika Tarehe 3/4/2020, mahali dhamana ilipo Makumbusho yard. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

Kwa mawasiliano fika kwenye ofisi zetu Victoria 5th floor au piga.0652113262

115683302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO – MKUYUNI**
**MWANZA**

**MADAI PESA 17/2020**

**MARIAM ZACHARIA MALEKO……………MDAI**

**JANE MWEMA…………………………..MDAIWA**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mdai aliyetajwa hapo juu amefungua shauri dhidi yako kuhusiana na madai ya pesa unatakiwa kufika katika Mahakama hii mnamo tarehe 31/03/2020 saa 2:30 asubuhi kujibu madai yaliyotolewa dhidi yako.

**KUMBUKA KUWA:** Usipohudhuria siku hiyo shauri litasikilizwa na kuamuliwa bila wewe kuwepo.

Imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 26/03/2020.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO – MKUYUNI
MWANZA

115683702


**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# CHELSEA YAMWANIA NEUER WA BAYERN

**MUNICH,** Ujerumani

KLABU ya Chelsea imeripotiwa kwamba inawania kumsajili golikipa namba moja wa Bayern Munich, Manuel Neuer kipindi cha majira ya joto.

Huku majaliwa ya kipa wao, Kepa Arrizabalaga hayajulikani pale Chelsea, sasa kocha Frank Lampard anamwona Neuer kama ndio chaguo sahihi kwa upande wake.

Golikipa wa Barcelona, Marc-Andre ter Stegen pia amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka pale Camp Noun na Bayern ndio wanaotaja kumwania.

Chelsea wanataka kumsajili nahodha huyo wa Bayern kwa ajili ya kuimarisha safu yao na kwamba, Neuer mwenyewe anaonekana kutaka kuondoka kwa miamba hao wa Bavaria kwa mujibu wa gazeti la Bild.

Lampard ameripotiwa kuwa anataka kumwachia Kepa ambaye ni golikipa ghali zaidi duniani baada ya kuondoka kule Athletic Bilbao mwaka 2018 na kutua pale Stamford Bridge.

Chelsea wameamua kumwania Neuer kwa saababu kipa huyo wa kimataifa wa Ujerumani bado hajakubali kusaini mkataba mpya pale Bayern.

# Pedro: Sitaki kuondoka, natamani kubaki

**LONDON,** England

PEDRO amesisitiza kwamba alitaka kubakia Chelsea, akipuuzia taarifa kwamba anaondoka klabuni hapo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania mwenye umri wa miaka 32, awali alinukuliwa akisema kwamba, anaondoka Chelsea, baada ya mkataba wake kumalizika mwishoni wa msimu.

Pedro amesema ndoto yake ni kubakia kwa miamba hao wa Ligi Kuu England ingawa majaliwa yake bado hajajulikana.

"Kama watu wengi wanavyojua, mkataba wangu unamalizika Mei mwaka huu, lakini bado sijazungumza na kama nitaongeza mkataba mpya au nitaondoka," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Nimeona ujumbe mwingi kutoka kwa mashabiki wa Chelsea wakisema kwa heri na wakinishukuru kwa muda wangu niliokaa hapa, kitu ambacho nakubaliana nao.

"Lakini ningependa kuwaambia mashabiki wote kwamba mkataba wangu unakaribia mwisho, lakini bado ninatakiwa kuzungumza na klabu.






# Roberto asema alimtaka Neymar atue Real Madrid

**SAO PAULO,** Brazil

ROBERTO Carlos amebainisha kwamba, alimtaka nyota wa Brazil, Neymar pale Real Madrid muda "mrefu uliopita."

Neymar alijiunga na Paris Saint-Germain kutoka Barcelona mwaka 2017, lakini amekuwa akihusishwa na mpango wa kurudi pale Camp Nou huku pia kukiwa na uwezekano wa kwenda Real Madrid.

Carlos, gwiji wa Madrid na timu ya taifa ya Brazil, amesema alimtaka Neymar pale kwenye dimba la Santiago Bernabeu muda mrefu uliopita.

"Kama ingewa ni amri yangu, Neymar tayari angekuwa pale muda mrefu, lakini maisha ni tofauti na unavyotaka," alisema Carlos akiiambia Fox Sports Redio.

"Wachezaji wakubwa mara zote wanataka kucheza kwenye klabu bora duniani. Real Madrid leo hii ni mfano kwa kila mchezaji.

"Unataka kushinda Kombe la Ligi ya mabingwa Ulaya? Njoo Real Madrid."

Carlos alishinda mataji manne ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, na matatu ya Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Madrid, pia alishinda Kombe la Dunia mwaka 2002 akiwa na Brazil.

## Jesus anaweza kujiunga Juventus

**MANCHESTER,** England

GABRIEL Jesus anaweza kujiunga na Juventus siku za usoni, kwa mujibu wa mtu aliyempeleka pale Manchester City.

Fowadi huyo wa kimataifa wa Brazil mkataba wake wa sasa na City unamalizika mwaka 2023, lakini imebainika kwamba, anaweza kuondoka mapema zaidi kama hatakuwa chaguo la kwanza la kocha, Pep Guardiola.

Jesus amekuwa kwenye wakati mgumu kupata namba kwenye kikosi cha kwanza, huku Sergio Aguero ndio akiwa namba 9 muhimu kwa kikosi hicho tangu alipotua City akitokea Palmeiras.

Kumekuwa na ripoti kwamba, Juventus wamekuwa wakiwania kumsajili fowadi huyo kwa ajili ya kuimarisha kikosi chao.

Na Giovanni Branchini, wakala ambaye alimsaidia Jesus kutua pale Etihad, alisema kuna uwezekano mkubwa kwa mteja wake huyo kuondoka wakati wa kipindi cha majira ya joto.

Alipoulizwa na gazeti la Calciomercato kama anafikiri Jesus anaweza kuhamia Juventus kwa siku za usoni, Branchini alijibu: “Tunazungumza kuhusu mwanasoka mkubwa na klabu kubwa, kila kitu kinawezekana.







## UNITED KUANZA KULONGA NA POGBA

**MANCHESTER,** England

REAL Madrid inatakiwa kuharakisha kumsajili Paul Pogba kwani sasa Manchester United inapanga kuanza mazungumzo ya kumwongezea mkataba mpya, kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail.

Pogba kwa muda mrefu amekuwa akiwaniwa na Real, huku kocha Zinedine Zidane akionesha wazi kuvutiwa nae, na awali walijaribu kumsajili kiungo huyo mwaka 2016.

Sasa kwa mujibu wa gazeti la AS, wanatakiwa kuongeza nguvu kumsajii kipindi cha majira ya joto kama wanamtaka pale kwenye dimba la Santiago Bernabeu.

Mkataba wa sasa wa Pogba pale United unamalizika kipindi cha majira ya joto cha mwaka 2021, ingawa United wanakipengele cha kumwongezea mwaka mmoja zaidi.

Lakini gazeti la AS limeripoti kwamba, kama United wakifanikiwa kumwongezea mkataba Pogba itakuwa kazi ngumu kwa Real Madrid kumnasa.

Kama hiyo ikitokea, maana yake ni kwamba, Real Madrid watatakiwa kumsubiri Pogba hadi mwaka 2022.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 ambaye ni mshindi wa Kombe la Dunia, msimu huu amekuwa akisumbuliwa na majeruhi ya mara kwa mara na sasa anapigania kupona kifundo cha mguu kilichomweka nje ya dimba kwa miezi kadhaa.

## *Sio haki Messi kutoshinda Kombe la Dunia - Ustari*

**BUENOS AIRES,** Argentina

LIONEL Messi kutoshinda taji la Kombe la Dunia na Argentina haitakuwa haki, kwa mujibu wa golikipa Oscar Ustari.

Ustari ni golikipa wa kimataifa wa Argentina ambaye anacheza soka la kulipwa katika klabu ya C.F. Pachuca ya nchini Mexico.

Messi ameshinda karibia kila kitu kwenye soka akiwa kama mchezaji wa Barcelona - kuanzia Ligi ya Mabingwa Ulaya, LaLiga, UEFA Super Cup, klabu bingwa ya Dunia, Copa del Rey na Supercopa de Espana.

Hata hivyo, mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or bado hajafanikiwa kubeba kombe akiwa na jezi ya timu ya taifa ya Argentina baada ya kumaliza kama mshindi wa pili wa Kombe la Dunia mwaka 2014, pia akicheza fainali mbili mfululizo za Copa America mwaka 2015 na 2016.

Na sasa golikipa Ustari anaona kwamba sio haki kwa nahodha Messi - ambaye ni mfungaji wa wakati wote wa nchi hiyo kutoshinda Kombe la Dunia.

“Sina shaka kama Messi ni bora duniani, lakini haitakuwa haki kwa Messi kutoshinda Kombe la Dunia,” amesema Ustari akiiambia redio Radio Mitre.

“Kumtilia shaka Messi ni ujinga. Mambo yanaweza kwenda sawa au la, lakini naweza kuwaambia kwamba nilimwona akilia kama mtoto kwa sababu ya kile kinachotokea kwenye timu ya taifa. Ni ngumu sana kuvaa viatu vyake.”



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# UNITED, SHANGHAI SHENHUA VITANI

## ●●● Ni katika kuwania saini ya Ighalo, klabu yake hiyo 'mama' ya zamani yaandaa ofa...

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United inakabiliwa na upinzani mkali katika kumsajili Odion Ighalo baada ya mchezaji huyo anayecheza hapo kwa mkopo kupewa ofa nono ya kuongeza mkataba wake na klabu yake 'mama', Shanghai Shenhua ya nchini China.

**Mkataba wa muda mfupi wa mkopo wa Ighalo pale Old Trafford unamalizika Mei 31, mwaka huu.**

United imeripotiwa ipo tayari kumsajili nyota huyo wa kimataifa wa Nigeria kwa kitita cha pauni milioni 15 ili aendelee kuwachezea miamba hao wa Ligi Kuu England.

Hata hivyo, klabu yake ya Shanghai Shenhua imetoa ofa ya kumwongezea mkataba wa miaka miwili na mshahara wa pauni 400,000 ambao utamfanya achezee kule nchini China hadi Desemba mwaka 2024.

Ighalo ambaye amekuwa na mwanzo mzuri wa kucheza pale United, sasa yupo njia panda ama kukubali kupewa mkataba wa kudumu au kuongeza mkataba na klabu yake ya zamani.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, ambaye amefunga mabao manne katika mechi nane alizocheza, anaonekana kwamba anataka kubakia Manchester United.

Awali wengi walitilia shaka usajili wa United kwa mchezaji huyo wakati wa siku ya mwisho ya kufungwa kwa pazia la dirisha dogo la Januari, lakini kiwango chake kimewaziba midogo na sasa mashabiki wanataka mchezaji huyo apewa mkataba wa kudumu.

United walipomchukua Ighalo kwa mkopo walikubali kulipa sehemu ya mshahara wake wa pauni 300,000 kwa wiki ambao wao walikuwa wakitoa pauni 130,000.

Lakini sasa Shanghai imewashangaza United baada ya kutoa ofa nene ya kutaka kumlipa mshahara wa pauni 400,000 kwa wiki, mshahara ambao United wameripotiwa kutokuwa tayari kuutoa.

Thamani ya Ighalo kwa sasa kama United wanataka kumnunua moja kwa moja ni pauni milioni 15.

Hata hivyo, kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail, Ighalo ndoto zake ni kuendelea kucheza pale Old Trafford hata kama atapunguziwa mshahara wake.

Tangu Ighalo alipotua United amepewa jukumu la kuongoza safu ya ushambuliaji ambayo inawakosa, Marcus Rashford aliye majeruhi na Romelu Lukaku ambaye ameuzwa Inter Milan.

## ZISIKUPITE

### MADRID YAMTAKA HAALAND

REAL Madrid imetangaza nia ya kumsajili mshambuliaji, Erling Braut Haaland (19), wa Borussia Dortmund katika kipindi cha majira ya joto. Straika huyo wa Timu ya Taifa ya Norway alijiunga na vigogo hao wa Bundesliga majira ya joto yaliyopita na dau lake la uhamisho lililowekwa katika mkataba ni pauni milioni 50. ***(Standard)***

### EPL KUREJEA KARIBUNI

KLABU zinazoshiriki Ligi Kuu England zimeelezwa zitarejea katika harakati za soka kuanzia Aprili 30, mwaka huu na tarehe mpya ya kuanza kwa michezo mbalimbali itatangazwa wiki ijayo kufuatia kuimarika kwa maambukizi ya virusi vya corona (COVID 19). ***(Mail)***

### POGBA ATAKIWA UNITED

MANCHESTER United inajiandaa kumwongeza mkataba Paul Pogba (27), lakini uamuzi huo utamweka "njia panda" mshindi huyo wa fainali za Kombe la Dunia akiwa na kikosi cha Ufaransa. ***(AS - in Spanish)***

### PEDRO KUONDOKA CHELSEA

KIUNGO Mhispania Pedro (32), amesema ataondoka Chelsea mwishoni mwa msimu huu baada ya mkataba wake na klabu hiyo maarufu The Blues kumalizika. ***(Independent via Cadena Ser)***

### EVERTON YAINGIA VITANI

EVERTON imeungana na klabu nyingine nne kuwasilisha ofa ya kumwania beki wa Lille Mbrazili Gabriel (23), ambaye thamani yake imeelezwa kuwa ni pauni milioni 30. ***(Sky Sports)***

### NDOMBELE ANUKIA BARCA

BARCELONA imetangaza nia ya kumsajili mchezaji ghali wa Tottenham, Tanguy Ndombele (23), ambaye alijiunga na klabu hiyo ya London Kaskazini kwa dau la pauni milioni 55 akitokea Lyon majira ya joto mwaka jana. ***(Mundo Deportivo via Star)***

### SPURS, SKIPP WATETA

MABOSI wa Tottenham wameanza mazungumzo ya awali na kiungo raia wa England, Oliver Skipp (19), kwa ajili ya kumpa mkataba mpya wa muda mrefu wa kuitumikia klabu hiyo. ***(Football Insider)***

### MELAMED AGEUKA LULU

CHELSEA, Real Madrid, Barcelona na Bayern Munich zote zimeonyesha nia ya kumsajili kiungo chipukizi wa Espanyol na Timu ya Taifa ya Vijana ya Hispania, Nico Melamed (18), ambaye thamani yake imetajwa kuwa ni pauni milioni 7.3. ***(Gianluca Di Marzio - in Italian)***

### KARIUS AGOMBEWA ULAYA

WEST Ham, Sporting Lisbon na Anderlecht ni baadhi ya klabu ambazo zimeonyesha nia ya kumsajili golokipa wa Liverpool na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Loris Karius (26), ambaye yuko kwa mkopo katika klabu ya Besiktas. Thamani ya nyota huyo anayemaliza mkataba wake mwishoni mwa msimu huu ni pauni milioni 4.5. ***(Voetbal24 - in Dutch)***

### SOLER AKARIBIA ARSENAL

ARSENAL imejiandaa kuwania saini ya kiungo wa Valencia na Timu ya Taifa ya Hispania, Carlos Soler (23), huku klabu hiyo ya La Liga ikijipanga kuuza wachezaji wake ili kuweka sawa kumbukumbu zao za fedha kwa mujibu wa kanuni za usajili. ***(Sky Sports)***

HABARI MICHEZO

## Polisi Tanzania yafikiria 'Top 5'

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Polisi Tanzania umesema klabu hiyo imedhamiria kutimiza malengo yake iliyoweka katika msimu wa Ligi Kuu Bara ambayo inaelekea ukingoni, imefahamika.

Makamu Mwenyekiti wa timu hiyo, Robert Munisi, alisema kwa kushirikiana vema na benchi la ufundi ili kufanya vizuri katika michezo tisa iliyobakia na hatimaye kumaliza kwenye nafasi ya tano katika msimamo wa ligi hiyo.

Munisi alisema kufikia malengo hayo wachezaji wanalazimika kupambana kutafuta ushindi katika michezo yao.

Alisema kwa kipindi hiki cha mapumziko benchi la ufundi limetoa programu zake kwa wachezaji, wanaporejea wanakuwa fiti na kuendelea na mapambano ya kuhakikisha wanapanda hadi nafasi ya tano.

"Kwa sasa tupo nafasi ya sita, malengo yetu makubwa ni kutopoteza mechi nyumbani na kwenda kupambana kusaka pointi nyingine ugenini," Munisi alisisitiza.

Alizitaja mechi zao tano za ugenini zilizobakia ni dhidi ya Mbao FC, Alliance FC, Kagera Sugar, Biashara United, Mbeya City na Tanzania Prisons.

## KMKM yatamba kutwaa ubingwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAKATI mabao 333 yamefungwa katika michezo 168 ya Ligi Kuu Zanzibar, Kocha Mkuu wa vinara wa ligi hiyo, KMKM, Ame Msimu, amesema matarajio na malengo yao ni kutwaa taji hilo msimu huu.

Ligi Kuu Zanzibar inayoshirikisha klabu 16, nayo imesimama kutokana na amri ya serikali kwa lengo la kupambana na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19).

Msimu alisema licha ya nchi kukabiliwa na kipindi kigumu ikiwamo wachezaji kutofanya mazoezi kwa pamoja kutokana na janga la corona, lakini bado anaamini timu yake itafanya vizuri katika mechi zilizosalia na hatimaye malengo yao kukamilika.

Alisema amejiandaa kukutana na changamoto ya kurejesha viwango vya wachezaji wake baada ya kuanza mazoezi ya pamoja kwa sababu ni ngumu kurejea wakiwa kwenye ubora walioku-wa nao awali kabla ya ligi haijasimama.

"Ligi itakapoendelea tena kutakuwa na changamoto ya mazoezi, hili haliepukiki, kwa sababu timu nyingi zilivunja kambi, lakini hata kama wachezaji wamezoea kucheza soka, suala la kufanya mazoezi lazima litakuwa na mapungufu," Msimu alisema.

Aliongeza changamoto hiyo ya kulinda viwango inatokana na wachezaji kutokuwa na uwezo wa kununua vifaa vya mazoezi ya viungo kama ilivyo na nyota wenzao wanaocheza katika mataifa na klabu nyingine duniani.

# WAWA AWAAMBIA YANGA WASAHAU UBINGWA BARA

**Na Saada Akida**

BEKI wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Pascal Wawa, amesema mapumziko yanayoendelea hayatawafanya warudi nyuma na badala yake wanajiimarisha zaidi ili kufikia malengo yao ya kutwaa ubingwa wa msimu huu wa mwaka 2019/20.

**Wawa aliliambia gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, kuwa wanatumia vizuri mapumziko kurekebisha upungufu walioubaini katika mechi zilizopita na kujiweka imara kuwakabili wapinzani wao.**

Beki huyo wa zamani wa Azam FC alisema wanajiandaa kuendeleza kasi ya ushindi kama waliyokuwa nayo kabla ya ligi kusimama licha ya ushindani uliopo katika kila mchezo.

Alisema Simba ina mikakati ya kuhakikisha wanatwaa ubingwa wa ligi hiyo kwa mara ya tatu mfululizo, hivyo mapumziko haya yanayoendelea wanayatumia kutekeleza programu maalumu walizopewa na benchi la ufundi.

"Huku tukiwa na malengo yetu ya kufanya vizuri kwa kutwaa ubingwa kwa mara nyingine, muda huu wa mapumziko tunautumia kwa ajili ya kujiweka fiti kwa kufanya mazoezi ili tutakaporejea tuendelee na makali yale yale, moto ule ule," alisema Wawa.

Aliongeza kuwa katika nafasi ya kwanza kwenye msimamo wa ligi haitawafanya kubweteka kwa sababu timu nyingine zilizoko chini yao zinapambana kufika katika nafasi hiyo ya juu.

"Ligi ipo katika ushindani mkubwa, kufikia malengo yanayotarajiwa ni lazima tupambane kuhakikisha tunafanya vizuri katika michezo yetu ya mwisho ya kumaliza msimu," alisema Wawa.

Simba ikiwa inaongoza ligi ikiwa na pointi 71 na safu ya ulinzi ya timu hiyo iliyoko chini ya beki huyo raia wa Ivory Coast imeruhusu mabao 15 katika mechi 28 walizocheza.



Wachezaji wa timu ya Vetenari Veterans, wakifanya mazoezi kwenye Uwanja wa Mwembe Yanga Temeke jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Tshabalala bado aikumbuka Vita

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI timu yake ikiwa inaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Bara, beki wa Simba, Mohammed Hussein 'Tshabalala', amesema bado anaikumbuka mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya AS Vita kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Simba ilitinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika mwaka juzi baada ya kupata ushindi wa mabao 2-1, dakika ya lala salama na kuwaondoa Wakongomani hao.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam, Tshabalala alisema hataisahau mechi hiyo ambayo tayari mashabiki na wadau wa soka nchini waliamini Simba imeshatolewa katika michuano hiyo.

Beki huyo alisema Simba ilicheza katika kiwango cha juu na kila mchezaji alionyesha wanahitaji kusonga mbele na uwezo wa kufanya hivyo wanao.

'Sitakaa nije kuisahau mechi ile, nimeshacheza michezo mbalimbali yenye ushindani na yenye historia, lakini mechi ya AS Vita ilikuwa ni zaidi, nitabaki kuikumbuka katika maisha yangu yote," Tshabalala alisema.

Simba ndio mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, lakini msimu huu walitolewa mapema kwenye mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Bingwa wa Ligi Kuu ndio ataiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kinara wa michuano ya Kombe la FA atapata tiketi ya kushiriki mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Michezo
Jumamosi Machi 28, 2020
Nipashe



United, Shangai Shenhua vitani UKURASA 30



Mshambuliaji wa Valencia, Ferran Torres (kulia), akipambana kuwania mpira dhidi ya nyota wa Barcelona. Torres (20) yuko katika rada za Liverpool, Real Madrid na Barcelona katika majira ya joto. **PICHA: MTANDAO**

# Senzo: Simba itasajili kisasa

## ●●● Aeleza haitakurupuka katika mchakato huo, aweka wazi wa kuwatoa kwa mkopo...

**Na Somoe Ng'itu**

KUELEKEA msimu ujao na kukabiliana na ushindani katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, uongozi wa Simba ya jijini Dar es Salaam umesema hautafanya usajili wa kukurupuka au 'mihemko'.

**Simba yenye pointi 71, ndio mabingwa watetezi na vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa wamepoteza mechi tatu kati ya michezo 28 waliyocheza msimu huu.**

Akizungumza na Nipashe jijini jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Senzo Mazingisa amesema klabu hiyo imejiandaa kusajili wachezaji wenye viwango vya juu kutoka katika ligi zenye mafanikio hapa barani Afrika na kwa kutumia kampuni zenye uzoefu na kazi hiyo.

Senzo alisema wanahitaji wachezaji ambao wana uwezo na uzoefu wa kupambana katika mashindano ya kimataifa na kamwe Simba haiangalii mechi za Ligi Kuu Bara au michuano ya Kombe la FA pekee.

"Katika suala la usajili tumeshaanza skauti katika maeneo mengi hapa barani Afrika ili kupata wachezaji bora na imara, pengine tutafanya usajili mzuri kuliko misimu yote kwa sababu tutaangalia vigezo vingi kulingana na mahitaji yetu," alisema Senzo.

Ofisa huyo alisema katika kukamilisha mchakato wa kusajili wachezaji wapya, klabu itazingatia zaidi ripoti ambayo itaeleza wazi ubora na upungufu alionao mchezaji husika kabla ya kufanya uamuzi wa kumpa mkataba.

Kiongozi huyo ameweka wazi katika kuendeleza vipaji kwa faida ya nchi, Kocha Mkuu Sven Vandenbroeck ametoa baraka ya kutolewa kwa mkopo kwa wachezaji ambao wanakosa namba katika kikosi chake au kuruhusiwa kujiunga na klabu nyingine kwa wale waliomaliza mikataba yao ndani ya Simba.

"Katika ligi ya hapa ndani tunaweza kusajili wachezaji kama wawili, na waliobakia tutaangalia kwenye nchi nyingine za Afrika, ambazo zimeendelea kisoka, hii itatusaidia kutimiza malengo yetu," Senzo alisema.

Aliongeza kwa kuwataka wachezaji wa timu hiyo kuendelea na mazoezi binafsi wakiwa majumbani kwao katika kipindi hiki cha mapumziko yaliyotolewa kutokana na kupambana na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19), ambao ni janga lililoenelea sehemu mbalimbali duniani.

# Bundi aendelea kuzunguka Yanga

**Na Saada Akida**

IKIWA imepita siku mbili baada ya mambo kuwekwa sawa kati ya uongozi wa Yanga na wadhamini wao, Kampuni ya GSM, Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Yanga, Shija Richard, ametangaza kujiuzulu nafasi zote alizokuwa anazishikilia katika klabu hiyo.

Taarifa zilizopatikana jijini Dar es Salaam jana zinaeleza Shija ameamua kuchukua uamuzi huo wa kujiweka pembeni kwa hiari yake, lakini anaahidi wakati muafaka ukifika ataweka wazi kilichopelekea kuchukua uamuzi huo.

Chanzo chetu kilisema Shija ameamua kujiuzulu kwa sababu anafahamu Yanga ni kubwa kuliko yeye na uamuzi huo kwa sasa utaisaidia klabu yao.

"Lakini amesema yamezungumzwa mambo mengi katika kipindi hiki, ila yeye hatazungumza chochote mpaka wakati wa kufanya hivyo utakapofika, ndio atazungumza", kilisema chanzo chetu.

Shija anatajwa kuwa mmoja wa viongozi waliokuwa wanapinga namna GSM ilivyokuwa inafanya majukumu ya klabu badala ya kufuata makubaliano yaliyomo kwenye mkataba.

# Niyonzima aahidi 'dozi' zitaendelea

**Na Shufaa Lyimo**

KIUNGO wa kimataifa wa Yanga, Haruna Niyonzima, amewataka wachezaji wenzake kufuata vema programu zote za mazoezi walizopewa na Kocha Mkuu wa kikosi hicho, Luc Eymael, ili watakaporejea kwenye Ligi Kuu Bara waendeleze 'dozi'.

Akizungumza na gazeti hili jana, Niyonzima alisema ni wajibu wa kila mchezaji kufanya mazoezi ili kujiweka sawa na tayari kwa kukabiliana na ushindani.

Niyonzima alisema mechi zote za Ligi Kuu Bara zilizobakia na mashindano ya Kombe la FA ni ngumu kwa sababu timu zote zinahitaji kupata matokeo chanya.

"Nashauri wachezaji wenzangu kujituma na kufanya mazoezi ili kuiweka miili sawa katika kipindi hiki cha mapumziko, tunahitaji kurejea na nguvu na si kuanza upya", alisema Niyonzima.

Mnyarwanda huyo alisema endapo mchezaji yoyote atakaa bila ya kufanya mazoezi, atajiweka kwenye wakati mgumu mara mechi za Ligi Kuu Bara zitakaporejea tena.

"Nafahamu athari za kutokufanya mazoezi, nikikaa bila mazoezi mwili utakuwa mzito na mwisho wa siku nitashindwa kutumikia timu yangu katika kiwango kizuri", Niyonzima alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >